SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**CCM** yaibuka kidedea Ushetu, ACT yatoa neno ushindi Konde

UKURASA 4


# Nipashe

Jumatatu Oktoba 11, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580730

www.ippmedia.com

MWANGA WA

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




Tyson Fury amchapa Wilder kwa KO

UKURASA 22

# Rais Samia aanika mafanikio miezi 6

• **Asema** miradi ya JPM itatekelezwa, aonya ulaji fedha za Uviko... *Endelea Uk.2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akihutubia taifa kwenye uzinduzi wa Kampeni ya Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya Uviko-19 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Mhagama ataka waajiri kutumia fursa msamaha tozo michango NSSF

UKURASA 4




Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, akimkabidhi Tuzo ya Mkurugenzi Mtendaji Bora wa Mwaka, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, katika hafla ya kugawa tuzo hizo zinazofahamika "The Top 100 Executive Award" jijini Da es Salaam. Tuzo hizo zimeratibiwa na Kampuni ya EasrernStar. **Habari Uk.8. NA MPIGAPICHA WETU**

## Matukio siku 42 kesi ya Freeman Mbowe

UKURASA 3

**MICHEZO** **MBUNGE WA RORYA AJITOSA UMOJA CUP** UK.20 **MAONI, KATUNI** UK.6

# ...Aonya watakaoiba fedha za Uviko-19

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amewaonya watakaodokoa fedha za Uviko-19 zilizotolewa kwa ajili ya kukabiliana na athari za corona kuwa watajua rangi yake halisi na hatakuwa na huruma na mtu.

Aidha, amemwagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha hizo ili zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa na thamani halisi.

Samia aliyasema hayo jana alipokuwa akizindua Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano ya Uviko-19 jijini hapa.

Alionya uundaji wa utitiri wa kamati za kusimamia fedha hizo na kwamba iundwe kamati ya wataalamu kwenye mikoa watakaosimamia hadi wilaya na chochote kitakachotokea watabanwa wao.

"Kamati zikiwa ndogo tutaweza kushika mtu. Hili niliseme tu kwa wale watakaotaka kujua rangi zangu halisi, mkinitizama hivi mnasema Mheshimiwa Rais ni mweupe, lakini nina rangi halisi, kwa hiyo kwa wanaotaka kuzijua rangi zangu wajaribu kudokoa fedha hizi au wabadilishe matumizi bila maelewano."

"Ukiangalia programu hii nchi inakwenda kuchemka kila kona itakuwa na miradi ya maendeleo, niwatake wakurugenzi wa halmashauri na timu zao kwenda kusimamia ipasavyo, kwenye fedha hii sina huruma na mtu kwa sababu, nina uwezo wa kupata mikopo mingine tukivurunda hapa tutakuwa tumejitia doa."

"Sitakuwa na huruma na mtu atayechezea fedha hii kuanzia mawaziri wangu, chini kwa wakurugenzi na wanaowafuata niwaombe mkasimamie vyema miradi hii," alisema.

Alisisitiza: "Utaratibu wa manunuzi wa single source uruhusiwe kutumiwa kwenye ununuzi wa vifaa kwa kuwa ukitumika mchakato wa ununuzi wa zabuni utatuchelewesha na kuchukua muda mrefu mpango wenyewe ni wa miezi tisa."

Alimwagiza Waziri wa Fedha na Mipango kuhakikisha urasimu wa misamaha ya kodi kwa vifaa vitakavyoagizwa nje ya nchi kwenye utekelezaji wa mpango huo uondolewe.

Alisema mpango huo utagharimu fedha nyingi na upatikanaji wake ulikuwa na mbinu mbalimbali, huku akisema nchi nyingine zilielekeza kwenye ununuzi wa chanjo na vifaa, lakini Tanzania imejielekeza kwenye miradi ya kusaidia kutoa huduma.

Aidha, alisema mbali na Shirika la Fedha Duniani (IMF) kutoa fedha za kukabiliana na athari za Uviko-19, Serikali ya China, Benki ya Dunia na Umoja wa Ulaya wameonyesha nia kuunga mkono utekelezaji wa mpango huo.

"Baada ya kupata fedha hizi hawa nao tupo kwenye mazungumzo wataingiza tena fedha kwenda kwenye maeneo mengine au kukuza maeneo hayo, tunawakaribisha wadau wengine waingie kwenye mpango huu," alisema.

**UKAGUZI FEDHA MIRADI MIKUBWA**

Rais Samia alisema serikali inajiandaa kufanya ukaguzi fedha zote zilizotumika kwenye miradi ya maendeleo kulingana na ujenzi halisi unaofanyika kwenye miradi yote mikubwa.

Alisema miradi ya kimkakati ni urithi ulioachwa na Hayati John Magufuli na miradi yote inaendelea kutekelezwa na kwa kipindi cha miezi sita ujenzi wa SGR Dar es Salaam hadi Morogoro imefikia asilimia 93 huku Morogoro hadi Makutupora imefikia asilimia 70.

"Tumeanza kipande cha Mwanza hadi Isaka ambapo kiasi cha Sh. trilioni 1.3 kimetumika, usafiri wa maji Septemba mwaka huu tumekamilisha ujenzi wa gati moja kwa Bandari ya Dar es Salaam na kazi ya kuchimba na kutanua kuongeza kina imeanza mwezi huo, ujenzi Bandari Kavu Kwala umefikia asilimia 58 na ujenzi wa meli mpya Ziwa Victoria umefikia asilimia 80.1."

"Mwezi Juni 2021, serikali ilisaini mikataba mitano kwa ajili ya ukarabati wa meli ya mabehewa ya MV Umoja, ujenzi wa meli ya kubebea mabehewa na mizigo kwenye Ziwa Victoria, meli mpya ya mizigo na ya abiria Bahari ya Hindi na meli ya kubeba mafuta Ziwa Tanganyika, yote inathamani ya Sh. bilioni 317.4," alisema.

Alisema ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato mkataba umesainiwa na upanuzi wa viwanja vingine unaendelea huku ndege tatu zilizonunuliwa na serikali zote zimewasili na kuwa na ndege 11 na imetia saini mkataba wa kununua ndege nyingine tano ikiwamo Dream Liner moja, Boeing mbili, ndege ya mizigo moja na ndege ya Bombardier moja ambazo zote zina thamani ya Sh. bilioni 596.3 zimetolewa.

Rais Samia alisema ujenzi wa barabara ya mzunguko ya njia nne Dodoma umeanza na barabara ya njia nane ya Dar es Salaam inaendelea na ipo hatua za mwisho kukamilika.

"Ujenzi wa madaraja makubwa Kigongo, Busisi, Wami unaendelea vyema, ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere la kufua umeme limefikia 55.6 na Sh. bilioni 596.7 zimetumika kati ya mwezi Aprili hadi Septemba, umeme umepelekwa kwenye vijiji 312 na vijiji vilivyosalia vitafikishiwa umeme ifikapo Desemba mwakani,"alisema.

Alisema Sh. bilioni 259 zimetolewa kwenye ujenzi wa bomba la mafuta ili kununua hisa za umiliki wa bomba hilo.

Alisema yatajengwa masoko kwa ajili ya machinga ili kupanga miji na majiji.

**RAIS MWINYI**

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, alisema atahakikisha kunakuwapo na nidhamu ya matumizi ya fedha hizo ambazo Zanzibar imepata Sh. bilioni 230.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, akikabidhi tuzo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Tanga Cement PLC, Reinhardt Swart, kampuni hiyo iliibuka mshindi wa kwanza wa jumla wa tuzo za Rais za Wazalishaji Bora wa Viwandani mwaka 2020/2021. Hafla hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya CTI, Paul Makanza, Waziri wa Viwanda na Biashara, Kitila Mkumbo na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla.

# Rais Samia aanika mafanikio miezi 6

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameweka wazi mafanikio mbalimbali yaliyopatikana ndani ya kipindi chake cha miezi sita ya uongozi huku akisema haikuwa mepesi.

Akizungumza jana na wananchi kwenye uzinduzi wa Kampeni ya Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano ya Uviko-19, Rais Samia alisema "Pamoja na kwamba nilikuwa makamu wake na wengine tulikuwa serikalini ukweli ni kwamba tulikuwa hatujajiandaa kwa lile, zaidi ya hapo Hayati Magufuli alikuwa kiongozi mahiri na jasiri hivyo basi si rahisi kuvaa viatu vyake, viatu vyake bado ni vikubwa kwangu."

"Nilipokuwa nakabidhiwa uongozi wimbi la pili la corona lilikuwa limeshika kasi hivyo hatukujua tuanzie wapi, ndiyo maana katika hotuba niliyotoa niliwaomba sana tuwe watulivu, kudumisha umoja na mshikamano na kuwa kitu kimoja, niwashukuru Watanzania kwa kunielewa na hatimaye tukavuka kipindi kigumu."

Akitaja mafanikio hayo, Rais Samia alisema kwa kipindi cha miezi sita iliyopita amani na usalama imedumishwa, kero 11 za Muungano zimetatuliwa.

Aidha, alisema kwa kipindi hicho ukuaji wa pato la taifa kwa robo mwaka ya Aprili hadi Juni mwaka huu, uchumi umeongezeka hadi asilimia 4.3 ikilinganishwa asilimia nne mwaka uliopita na hadi Agosti 2021 akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Marekani bilioni 5.8 zilikuwa zinatosheleza kuagiza bidhaa nje ya nchi kwa miezi sita ikilinganishwa na Dola za Marekani Bilioni 4.9 kipindi kama hicho kwa mwaka uliopita.

Alisema kwenye ukusanyaji wa mapato kuanzia Aprili hadi Septemba 2021, Sh. trilioni 9.9 zimekusanywa, marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) Sh. bilioni 451.3, kulipa madeni nje ya nchi, kufanya uhakiki wa madeni ya ndani yanayofikia Sh. bilioni 439 yanayotokana na madai ya watumishi, wazabuni wakubwa na wadogo, makandarasi wakubwa, fidia, bima za ajali, madeni yameanza kulipwa na mengine yanaendelea kulipwa.

Kadhalika, alisema kuondolewa kwa urasimu wa upatikanaji wa vibali vya kazi na kwa sasa kuna mfumo ambao umepunguza muda wa kuomba kutoka siku 14 hadi siku moja au tatu endapo mwombaji atakamilisha taratibu zote na kukamilisha uundaji wa dirisha moja la uwekezaji la kielektroniki. Alisema kusajili miradi yenye thamani Dola za Marekani bilioni 3.5 ambayo itazalisha ajira 43,782 na kupunguza tatizo la ajira nchini, miradi 164 yenye thamani ya Dola za Marekani zaidi ya bilioni tatu imesajiliwa na Kituo cha Uwekezaji (TIC), ikilinganishwa na kipindi kilichopita huku usajili wa leseni za biashara 6,051 zimesajiliwa na BRELA.

"Tumefanya uhakiki wa mashamba yenye ukubwa wa hekta zaidi ya 237,000 na kupima afya ya rutuba ya udongo, kujenga vihenge na kukarabati kuanza ujenzi wa skimu za umwagiliaji, kudhibiti nzige, kuanzisha masoko, kufungua masoko nchi mbalimbali... kutoa Sh. bilioni 50 kwa NFRA na Sh. bilioni 50 kwa Bodi ya Mazao Mchanganyiko ambazo zimetoka Benki ya CRDB ili kununua mahindi kwa bei nzuri," alisema.

Alisema EPZA imetoa leseni kwa kampuni 18 na viwanda vidogo 374 vimeanzishwa huku leseni 5,126 zimetolewa kwa sekta ya madini ikilinganishwa na mwaka uliopita zilikuwa 3,195 kati yake tatu ni uchimbaji mkubwa na Sh. bilioni 335 zimekusanywa kwenye sekta hiyo.

"Kiwanda cha kusafisha dhahabu kimekamilika pale Mwanza na kuvuta VAT kwa wale watakaoleta madini ya dhahabu nchini kuingia kwenye kiwanda hicho," alisema.

Alisema idadi ya watalii imeanza kuongezeka kuanzia Machi hadi Septemba, mwaka huu 464,913 wametembelea nchini na jana kuna ndege kubwa imeingia nchini kutoka Ufaransa ikiwa na watalii 190 na itaenda Zanzibar.

Kuhusu ujenzi wa barabara, alisema kwa sasa wanatarajia kujenga barabara ya njia nne kutoka Dodoma kwenda Singida, Iringa, Dar es Salaam na Arusha.

Alisema kupitia TARURA Sh. bilioni 216.3 zimetumikia kufanya matengenezo ya barabara vijijini zilizoharibiwa na mvua msimu uliopita, pia Sh. bilioni 1.5 kwenye kila jimbo kwa ajili ya uwekaji wa lami huku kilometa 419 za mkongo wa taifa zikijengwa, kata 132 zimefikiwa na mawasiliano.

Alisema kuondoa VAT kwenye simu janja, vishkwambi imesaidia kuongeza watumiaji wa simu kutoka milioni 52 hadi kufikia milioni 55.4.

**WALIOCHANJA WAONGEZEKA**

Alisema hadi juzi takwimu zinaonyesha wananchi waliochanja Uviko-19 wamefikia 846,000 na hamasa inaendelea.

Pia serikali imejenga kiwanda cha vifaa vya kujikinga na ugonjwa huo ikiwamo kutengeneza barakoa na vifaa vingine huku Sh. bilioni 234 zikitumika kununua dawa, Sh. bilioni 7.9 kununua mashine ya kupasua ubongo bila kufungua kichwa katika Taasisi ya Moi.

**ELIMU BILA MALIPO**

Ndani ya miezi sita Sh. bilioni 145.58 zimetumika kugharamia elimu bila malipo na kwamba waliosema imekwenda watambue kazi inafanyika, Sh. bilioni 208 zimetumika kugharamia mikopo ya elimu ya juu, Sh. bilioni 120 kujenga miundombinu shule za msingi na sekondari.

Rais Samia alisema wananchi zaidi ya milioni mbili wamenufaika na utekelezaji wa miradi ya maji.

**WAFANYAKAZI**

Alisema watumishi zaidi ya 29,000 wameajiriwa, 100,830 wamepandishwa vyeo na kulipwa stahili zao, 8,802 wamebadilishiwa kada.

## HABARI KITAIFA

# Matukio siku 42 kesi ya Freeman Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

SIKU 42 za kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake watatu katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi zimetawaliwa na matukio kadhaa.

Miongoni mwa mambo hayo ni jaji kukataliwa siku ya saba ya kesi na kukubali kujitoa, aliyepokea kijiti kuteuliwa kuwa Jaji Kiongozi baada ya siku 29 tangu alipoanza kuisikiliza.

Jaji Elinaza Luvanda alianza kusikiliza kesi hiyo Agosti 31, mwaka huu, aliombwa kujitoa na akakubali Septemba 6 ikiwa ni siku ya saba na jaji aliyepokea kijiti Jaji Mustapha Siyani alianza kuisikiliza kesi Septemba 10 na Oktoba 8, mwaka huu, aliteuliwa kuwa Jaji Kiongozi ikiwa ni baada ya siku 29 tangu aanze kusikiliza kesi hiyo.

Kesi hiyo ilianza kusikilizwa mahakamani hapo Agosti 31, mwaka huu, ambapo hadi kufikia leo ni takribani siku 42.

Agosti 31, mwaka huu, jopo la mawakili 14 waliokuwa wanamtetea Mbowe na wenzake watatu waliomba Mahakama iwaachie huru wateja wao kwa sababu Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi haina mamlaka ya kusikiliza makosa ya ugaidi.

Jamhuri walipinga kwa madai tafsiri si sahihi, Mahakama hiyo inayomamlaka ya kusikiliza shauri hilo.

Maombi ya pingamizi yaliwasilishwa mbele ya Jaji Luvanda, upande wa Jamhuri ulikwama kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali kwa sababu ya pingamizi.

Upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, Nassoro Katuga, Ignas Mwinuka, Esther Martin na Wakili wa Serikali Tilimanyo Magige.

Upande wa utetezi uliwakilishwa na Wakili Peter Kibatala, Jeremiah Mtobesya, John Mallya, Jebra Kambole, Frederick Kihwelo, Sisty Aloyce, Selemani Matauka, Nashon Mkungu, Michael Rugina, Bonifasia Makungu, Alex Maseba, Faraja Mangula, Michael Mwangasa na Gaston Shundu.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Halfan Bwire, Adam Kasekwa, maarufu Adam na Mohamed Ling'wenya, ambao wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kulanjama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei mosi na Agosti 2020.

Septemba mosi mwaka huu mahakama hiyo ilitupilia mbali pingamizi la mawakili wa utetezi na kusema kwamba inayo mamlaka kamili ya kusikiliza kesi za ugaidi.

Mvutano mwingine uliibuka baada ya uamuzi huo, upande wa utetezi ulipinga kusomwa kwa hati ya mashtaka kwa madai ina kasoro zisizorekebishika, wanataka mashtaka yaondolewe na washtakiwa waachiwe huru, huku Jamhuri wakipinga kwa madai hati ya mashtaka iko sahihi na waliomba pingamizi litupwe.

Septemba 6, mwaka huu, Jaji Luvanda alikubaliana na hoja moja ya pingamizi na kutupilia mbali hoja mbili.

Akitosoma uamuzi alisema msingi wa pingamizi ni makosa yaliyofunguliwa chini ya kifungu namba 4(3) cha Sheria ya Ugaidi namba 21 ya mwaka 2002, haikueleza malengo wakati ndio msingi wa makosa ya ugaidi kwa shtaka namba 1, 4, 6.

"Maoni yangu kwamba hoja hii inachukua muda mrefu sana, marejeo yalipaswa kufanywa katika hansad za Bunge, kuona michango ya wabunge wakati sheria hiyo inatungwa kuona kama walitoa tafsiri ya ugaidi bila kuhusisha itikadi za dini na siasa.

Alisema Mahakama inakubaliana na hoja moja ya upande wa utetezi kwamba shtaka namba 1, 4, 6 yaliyofunguliwa Chini ya Kifungu Namba 4(3) cha Sheria ya Ugaidi ilikuwa ni sharti kutumia maneno yaliyolengwa chini ya kifungu hicho.

Alisema anakubaliana na hoja ya Wakili Peter Kibatala kwamba ili kuweka tofauti hayo maneno yanaweka mpaka baina ya makosa ya ugaidi na makosa mengine ya jinai, hivyo alitupilia mbali hoja mbili na alikubali hoja moja akatoa maelekezo kwa upande wa Jamhuri kufanyia mabadiliko shtaka namba 1, 4 na sita.

Uamuzi ulipotolewa Mbowe aliomba Jaji Luvanda ajitoe kusikiliza shauri lao ili kujenga heshima yake, heshima ya Mahakama na asibebeshwe lawama ambazo pengine hazikustahili.

Alidai mawakili wao wanawasilisha vifungu mbalimbali vya sharia, lakini wanaona havitiliwi maanani ikiwamo katika pingamizi la kwanza kuhusu mamlaka ya mahakama.

"Hisia mbali mbali za jamii katika suala hili inaweza kuthibitisha katika mijadala inayoendelea katika Mtandao wa kijamii hatuwezi kupuuza," alidai Mbowe.

"Jaji Elinaza Luvanda ni mserikali na TISS, yuko Mahakama ya Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kimkakati, ameelekezwa kumfunga Mbowe huku Msajili akishughulika na CHADEMA, Rais atamwachia baada ya muda, kila pingamizi atalitupilia mbali haijalishi uhalali wake," alinukuu Mbowe maneno hayo yaliyoandikwa mtandaoni.

"Shauri lina maslahi mapana ya umma, naona ni busara nikae pembeni jaji mwingine aendelee nilipoishia.

Jaji Mustapha Siyani ambaye aliteuliwa kuwa Jaji Kiongozi, Oktoba 8 mwaka huu alipokea kijiti na kuanza kuisikiliza kesi hiyo Septemba 10, mwaka huu.

Mbowe na wenzake watatu walisomewa mashtaka na walikana kula njama kufanya ugaidi ikiwamo kumsababishia majeraha aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya.

Jaji Siyani alianza kusikiliza ushahidi wa shahidi wa kwanza Septemba 15, mwaka huu, ambaye ni Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi, Kinondoni, Kamishna wa Polisi Msaidizi, Ramadhan Kingai, alidai katika ushahidi wake kuwa alimsikia Luteni Denis Urio akisema mbele ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI), Robert Boaz kwamba kuna kundi la kihalifu linaandaliwa na Freeman Mbowe na kwamba wanataka kufanya vitendo vya kigaidi.

ACP Kingai alipotaka kutoa maelezo ya onyo ya Kasekwa kama kielelezo, Wakili Kibatala alipinga kupokelewa kama kielelezo kwa sababu anadai mteja wao aliteswa kabla na wakati wa kuchukuliwa maelezo hayo na kwamba yalichukuliwa zaidi ya saa nne.

Upande wa utetezi uliomba iwepo kesi ndogo ndani ya kesi ya msingi, mahakama ilikubali na mashahidi watatu upande wa mashtaka walitoa ushahidi wakionyesha kwamba mshtakiwa Kasekwa hakuteswa.

Septemba 17, mwaka huu Wakili Kibatala aliieleza mahakama kwamba wamebaini kuna mgongano wa kimaslahi, maelezo yanayodaiwa kutolewa na mshtakiwa wa pili Kasekwa yanawataja washtakiwa wengine na kuwahusisha na kesi ya ugaidi inayowakabili hivyo kila mshtakiwa aliyeyewa na wakili wake badala ya awali ambapo jopo lilikuwa likiwatetea washtakiwa wote.

Aliomba kutambulisha mawakili wa washtakiwa, alitaja mawakili 11 wanamtetea mshtakiwa wa nne, Mbowe peke yake.

Jaji Siyani alisikiliza mashahidi watatu wa upande wa Jamhuri na mashahidi watatu wa upande wa utetezi katika kesi ndogo ndani ya kesi ya msingi kuanzia Septemba 17 hadi Septemba 29, mwaka huu, ambapo upande wa utetezi walifunga ushahidi na mahakama kuamuru uamuzi utatolewa Oktoba 19, mwaka huu.

Wakati pande zote mbili zikisubiri tarehe ya uamuzi huo, Oktoba 8, 2021 Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania alimteua Jaji Siyani kuwa Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu.



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akiingia katika chumba cha Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Uhujumu Uchumi Sinza jijini Dar es Salaam jana, kusikiliza kesi inayomkabili. **PICHA: JUMANNE JUMA**


## TANGAZO LA KIFO



**DKT. BASIL A. SAPRAPASEN**

Familia ya Saprapasen kwa huzuni, tunasikitika kutangaza kifo cha Baba yetu Mpendwa **DKT. BASIL A. SAPRAPASEN** kilichotokea tarehe 07 Oktoba, 2021.

Msiba upo nyumbani kwa Marehemu Kinondoni mkabala na Bank ya Stanbic, Mtaa wa Mafinga, Kinondoni - Dar es Salaam.

Ibada Takatifu itafanyika katika Kanisa la **Mtakatifu IMMACULATA** UpangaDar es Salaam Jumatano, 13 Oktoba, 2021 saa 7:00 Mchana na Mazishi yatafanyika katika makaburi ya Kinondoni Dar es Salaam, saa 9:00 alasiri.

*2Timotheo 4:7*



## KUPOTEA KWA CHETI



116503802

**MOUREEN D MAKUNDI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3674-0027** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ST.JOSEPH MILLENIUM mwaka 2015, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa **DAR/CHA/RB/485789/2021**



## BANI INVESTMENT LIMITED
## DEBT COLLECTORS/ AUCTIONEERS

## NOTISI YA SIKU 14/TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **BENKI YA EQUITY** tunatoa notisi ya kulipa deni lenye dhamana tajwa hapo chini ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili.Vinginevyo tutafanya mnada wa hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| JINA LA MKOPAJI | JINA LA MMILIKI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|
| Ruvuma Contractors and General Supplies | Modesta Barnabas James | Nyumba yenye usajili RL. no.TMKO25731,yenye eneo la sqm 1532 | Mbagala kuu,wilaya ya Temeke -Dar es Salaam | 27.10.2021 | 4:00 asubuhi |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mali itauzwa "kama ilivyo " **as is where is basis"**
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki ni juu ya mnunuzi
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wowote isipokuwa usiku tu.

116501902

**Kwa maelezo zaidi wasiliana Na ofisi ya BANI INVESTMENT LTD Nkurmah Street, Lida Building, Ghorofa ya 3, Chumba No. 0313 S.L.P 71340 Dar es Salaam au kwa simu na. 0713 224 578.**

# Mhagama ataka waajiri kutumia fursa msamaha tozo michango NSSF

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, imewaomba waajiri wote nchini, kutumia fursa iliyotolewa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ya kutoa msamaha kwa waajiri wote wenye malimbikizo ya tozo zitokanazo na ucheleweshaji wa michango.

Waziri Jenista alisema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea Kiwanda cha Sukari Kagera kujionea uwekezaji mkubwa uliofanywa pamoja na kuangalia shughuli za NSSF zinazofanywa kiwandani hapo ikiwamo uwasilishwaji wa michango.

Alisema msamaha huo umeanza Oktoba mosi, mwaka huu na unahusu waajiri wote wenye malimbikizo ya michango na tozo kwa kipindi kinachoishia Juni 30, 2021 kwa kuzingatia vigezo mbalimbali.

"Niwaombe waajiri watumie hii fursa iliyotolewa na NSSF kwani huu ni utekelezaji wa maono ya Rais Samia Suluhu Hassan ambaye kila siku anatafuta mbinu ambazo zitarahisisha shughuli za uwekezaji nchini," alisema. Waziri Jenista alisema waajiri watakaolipa malimbikizo ya michango kuanzia Oktoba 2021 mpaka Novemba 31, 2021 watalipa msamaha wa tozo zitokanazo na ucheleweshaji wa michango husika kwa kiwango cha asilimia 100 jambo ambalo ni fursa kubwa kwa waajiri hao.

Alisema waajiri watakaolipa malimbikizo ya michango ifikapo Desemba 31, 2021 watapa msamaha wa tozo zitokanazo na ucheleweshaji wa michango husika kwa asilimia 75 na waajiri watakaolipa malimbikizo ya michango Januari 31, 2022 watapata msamaha wa tozo kwa kiwango cha asilimia 50.

"Niwaombe sana wawekezaji wote, waajiri wote nendeni mkashirikiane na NSSF kwenye ofa hii ambayo katika Mfuko tumeweza kupata msamaha huu hivyo tuitumie vizuri nafasi hii," alisema.

Aliishukuru NSSF kwa kuendelea kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wanachama na wadau ili kuhakikisha wanapata huduma nzuri na kutoa wito kwa waajiri wengine walio kwenye sekta binafsi kuhakikisha wanajisajili na kuwasajili wafanyakazi wao pamoja na kuwapelekea michango yao NSSF kwa wakati kwa kuwa hilo ni takwa la kisheria.

Awali, Katibu Tawala Mkoa wa Kagera, Profesa Faustine Kamuzora, aliupongeza Mfuko wa NSSF katika mkoa huo kwa kupunguza kero za wanachama na wadau kwa asilimia zaidi ya 90 kutokana na muda mrefu sasa uongozi wa mkoa huo kutopokea malalamiko yoyote ya wanachama wa NSSF.

Kaimu Mkurugenzi wa Uendeshaji wa NSSF, Cosmas Sasi, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko huo, Masha Mshomba, alisema Kiwanda cha Sukari cha Kagera kwa upande wa NSSF ni mdau mkubwa chenye wanachama 8,000 na kinachangia kila mwezi Sh. milioni 540.

Aidha, Mbunge wa Nkenge, Wilaya ya Misenyi mkoani Kagera, Florent Kyambo, alisema mwekezaji huyo licha ya kutengeneza ajira kwa Watanzania, ni mlipaji mzuri wa michango ya wafanyakazi wake NSSF.

Naye mwekezaji wa kiwanda cha sukari Kagera, Seif Seif alimshukuru Rais Samia kwa kuendelea kuwa na dira ya kukuza viwanda vya ndani na kuvilinda ili viweze kukua.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyakazi wenzake, Mhandisi Atugonza Phinis ambaye ni mwendeshaji mitambo kiwandani hapo, alisema kampuni ya Kagera imekuwa ikitoa ajira nyingi kwa vijana na kwamba wanafurahishwa na namna mwekezaji huyo anavyojali maslahi ya wafanyakazi wake kwa kuwasilisha michango NSSF ili pale watakapopatwa na janga waweze kunufaika na mafao mbalimbali yanayotolewa na mfuko huo.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mahagama (wapili kulia), akizungumza na uongozi wa Kiwanda cha Sukari cha Kagera alipotembelea kiwanda hicho mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Misenyi, Kanali Wilson Sekulo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM kidedea Ushetu, ACT yatoa neno ushindi Konde

**Na Wandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imemtangaza Emmanuel Cherehani kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa mshindi wa kiti cha ubunge Jimbo la Ushetu, mkoani Shinyanga kwa kupata kura 103,357 na kumshinda mpinzania wake, Mabula Julius wa ACT-Wazalendo aliyepata kura 3,588.

Katika uchaguzi huo, vyama vya siasa 16 vilijitokeza kuchukua fomu ya kugombea jimbo hilo, lakini vyama 14 vilikosa sifa na baadhi yao kushindwa kurejesha fomu mpaka muda ulipokwisha huku CCM na ACT-Wazalendo vikikidhi vigezo kwa wagombea wao.

Akitangaza matokea hayo, Msimaizi wa uchaguzi katika jimbo hilo, Limo Mwageni majira ya saa 11 alfajiri alisema, idadi ya wapiga kura walikuwa 165,418, lakini waliopiga kura walikuwa 107,188 katika vituo 457 vilivyokuwa vimeandaliwa katika jimbo zima.

Aidha, alisema idadi halali ya kura zilizopigwa zilikuwa 106,945, zilizokataliwa 243, huku mgombea wa Chama cha ACT-Wazalendo, Julius Mabula akipata kura 3,588 sawa na asilimia 3.4.

Kwa upande wake, mbunge mteule wa jimbo hilo, Emmanuel Cherehani, aliwashukuru wananchi wa jimbo hilo kwa kumchagua kuwa mbunge wa jimbo hilo na kuwaahidi kuyatekeleza yale aliyoawaahidi wakati akiwa jukwaani.

Mgombe wa ACT- Wazalendo, Mabula alisema kuwa kwa kampeni alizofanya katika jimbo hilo aliamini angeshinda na kuwa mbunge wa jimbo hilo, lakini imekuwa tofauti.

Uchaguzi mdogo wa jimbo hilo umefanyika baada ya aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo ambaye alikuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Elias Kwandikwa kufariki dunia Agosti 2, mwaka huu.

**ACT- WAZALENDO**

ACT-Wazalendo imesema endapo uchaguzi mkuu pamoja na nyingine ndogo zitafanyika kwa hali ya uhuru na kuzingatia haki kama ilivyofanyika kwa uchaguzi mdogo kwenye Jimbo la Konde Visiwani Zanzibar, hakuna watu watakaokuwa wanaumia au kuathirika.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Katibu wa Habari, Uenezi, Uhusiano na Umma ACT-Taifa, Salimu Bimani, wakat i akizungumza na Nipashe.

Alisema upungufu ulioonekana kwenye uchaguzi uliopita ikiwamo uchaguzi mkuu wa mwaka jana, haukuonekana kwenye uchaguzi wa Septemba 9, mwaka huu, jambo linalopaswa kuendelea.

"Kupitia uchaguzi huu mdogo wa Konde, tumebaini kwamba kumbe inawezekana kuendesha uchaguzi kwa kuzingatia haki na ukawa huru kwa vyama vyote vinavyoshiriki pasipo kusababisha athari," alisema Bimani.

"Katika uchaguzi huu mdogo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ilifanya kazi yake ambayo inatakiwa kufanya kwenye uchaguzi. Mambo mengi ya kutenda haki ambayo tumekuwa hatuyaoni katika chaguzi zilizopita, katika uchaguzi huu tumeyaona, hata kwenye kugawa vifaa vya uchaguzi safari hii na sisi tumeshirikishwa," alisema Bimani.

"Uchaguzi huu umefanyika vizuri, hatujaona magari wa washawa washa, wala watu kuzagaa ovyo kama ambavyo tumekuwa tukishuhudia katika chaguzi nyinginezo, waliokuwa wanaonekana vituoni ni askari wa kawaida tu na wale wanaosimamia uchaguzi, kwa kweli tunaipongeza NEC kwa hili, ndio maana hakukuwa na matukio ya watu kupigwa."

Pia alisema hata katika suala la mawakala, katika uchaguzi huo hawakupata changamoto zozote kama ambavyo imekuwa ikitokea katika chaguzi zilizopita.

**Imeandikwa Shaban Njia, KAHAMA na Elizabeth Zaya (DAR)**

## Hivi ndivyo Tril. 1.3/- zitakavyotumika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ametoa mchanganua wa kiasi cha Sh. trilioni 1.3 za Uviko-19 zilizotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) zitakavyoelekezwa kwenye sekta mbalimbali.

Akitoa jana maelezo kwenye uzinduzi wa Kampeni ya Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano ya Uviko-19, Mwigulu alisema fedha hizo zitajenga madarasa 15,000 ambayo yatalenga shule za sekondari na msingi 3,000 baada ya shule shikizi zilizochambuliwa na kuonekana zinasifa kuwa shule za msingi.

Aidha, alisema zaidi ya madawati 492,000 yatanunuliwa, kukamilisha vyuo vya VETA sita na vingine 26 ambavyo vilikwama kwa muda mrefu.

"Kujenga madarasa kwenye vyuo 17 vya ualimu, kuchapisha vitabu zaidi ya 10,000 vya nukta nundu," alisema.

Kuhusu sekta ya maji, Dk. Mwigulu alisema zimetengwa Sh. bilioni 46.2 kwa ajili ya maeneo ya mijini na Sh. bilioni 55.5 kukamilisha miradi ya maji vijijini ili kupambana na ugonjwa huo kupitia kunawa mikono.

"Kununua magari ya kuchimbia visima 25 na kila mkoa utakuwa na gari lake, kila ofisi ya RUWASA mkoa itakuwa na gari lake na maeneo yenye ukame, kununua mitambo ya kujengea mabwawa mitano kwa kila kanda, kununua seti nne za uchunguzi wa maji chini ya ardhi ili kupata maeneo sahihi ya kuchimba visima," alisema.

Aidha, Mwigulu alifafanua kuwa kwa sekta ya afya zimewekwa Sh. bilioni 466.9 kwa ajili ya hatua mbalimbali zinazolenga kukabiliana na ugonjwa huo.

"Tunaenda kujenga ICU kwa mpigo katika kila hospitali za rufani za mikoa, maalum na baadhi ya wilaya ambapo tunaongeza ICU 72," alisema.

Alisema ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za dharura za kisasa kwenye Hospitali ya Taifa, mikoa, baadhi ya wilaya zilizo kwenye maeneo ya kimkakati.

"Upatikanaji wa magari ya kubebea wagonjwa 20 za kisasa ambazo katika nchi yetu tumewahi kuwa nazo mbili tu na tunaenda kuongeza magari ya kubebea wagonjwa ya kawaida 375 kwa kila halmashauri na maeneo ya kimkakati yataenda kupata gari moja moja, na magari ya huduma za chanjo 214 kwa mpigo ili huduma hiyo ifanyike," alisema.

Pia alisema wataenda kuweka mfumo wa usambazaji hewa tiba Oksjeni na ununuzi wa mashine za X-Ray 85 na zitawekwa kwenye Hospitali ya Taifa, kikanda, mikoa yote na baadhi ya wilaya za kimkakati.

CT-Scan 29 zitawekwa kwenye Hospitali za Mikoa yote ili kuhakikisha huduma hiyo inapatikana na kwenye baadhi ya wilaya za kimkakati, hospitali za kanda zote zitakuwa na mashine za MRI.

# TANGAZO

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## PRESIDENT'S OFFICE-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
## KIBAHA DISTRICT COUNCIL

## FINANCIAL STATEMENTS FOR KIBAHA DISTRICT COUNCIL FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2020

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KIBAHA DISTRICT COUNCIL
STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE
FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2020

| | Notes | 2020 TZS | Restated 2019 TZS | Audited 2019 TZS |
|---|---|---|---|---|
| **Revenue** | | | | |
| Local taxes | 9 | 248,642,046 | 229,653,996 | 229,653,996 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 10 | 1,272,855,092 | 1,153,572,720 | 1,445,093,194 |
| Revenue from exchange transaction | 10 | 75,513,005 | 291,520,474 | |
| Amortisation of recurrent grants | 11 | 17,386,132,485 | 17,044,807,130 | 17,044,807,130 |
| Amortisation of capital grant | 23 | 1,948,295,480 | 3,824,237,433 | 3,824,237,433 |
| | | 20,931,438,108 | 22,543,791,754 | 22,543,791,754 |
| **Expenses** | | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 12 | 15,439,440,866 | 14,363,511,410 | 14,363,511,410 |
| Supplies and consumables used | 13 | 1,671,575,046 | 1,489,603,203 | 1,489,603,203 |
| Maintenance expenses | 14 | 352,025,417 | 127,403,979 | 127,403,979 |
| Grants and other transfer payments | 15 | 2,132,929,520 | 2,686,369,216 | 2,686,369,216 |
| Finance costs | 16 | - | - | - |
| Loss on Disposal of Asset | 8 | - | - | - |
| Provision for income not banked | 24 | 95,280,180 | - | - |
| Impairment Loss | 29 | 304,247,892 | | |
| Depreciation of property, plant and equipment | 29 | 718,742,752 | 1,861,410,595 | 1,861,410,595 |
| | | 20,714,241,673 | 20,528,298,403 | 20,528,298,403 |
| **Surplus/(deficit) during the year before adjustment** | | 217,196,435 | 2,015,493,351 | 2,015,493,351 |
| Own source fund contributed to capital grants | | - | - | |
| **Surplus/(deficit) during the year** | | 217,196,435 | 2,015,493,351 | 2,015,493,351 |

The financial statements were authorised for issue by the Full Council on 7th January,2021 and were signed on its behalf by:

Name: **Theopister K. Mrango** Title: **District Treasurer** Signature:______
Name: **Butamo N. Ndalahwa** Title: **Chairperson CMT** Signature:______
Name: **Ruth N. Mwelo** Title: **Secretary CMT** Signature:______

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KIBAHA DISTRICT COUNCIL
CASH FLOW STATEMENT
FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2020

| | Note | 2020 TZS | 2019 TZS |
|---|---|---|---|
| **Cash flows from operating activities** | | | |
| **Receipts** | | | |
| Local Taxes | 9 | 288,056,093 | 165,345,459.24 |
| Fees, Fines, Penalties and Licences | 10 | 1,206,171,939 | 1,153,572,719.64 |
| Other Ownsource Revenue | 10 | 75,513,005 | 291,520,474.29 |
| Grants Received | 11 | 17,289,315,894 | 16,949,075,808.85 |
| Development Grants | 23 | 1,631,803,612.75 | 3,265,100,000 |
| | | 20,490,860,544 | 21,824,614,462 |
| **Payments** | | | |
| Wages, Salaries and Employees Benefits | 12 | 15,318,526,455 | 14,363,511,410 |
| Supplies and Consumables Used | 13 | 1,183,947,229 | 1,319,064,217 |
| Maintanance Expenses | 14 | 305,865,455 | 127,403,979 |
| Grants and Other Transfer Payments | 15 | 2,098,147,020 | 2,686,369,216 |
| Finance Costs | 16 | - | - |
| **Total Payments** | | 18,906,486,158 | 18,496,348,822 |
| **Net cash from operating activities** | | 1,584,374,385 | 3,328,265,640 |
| **Cash flows from investing activities** | | | |
| Purchase of property, plant and equipment | 26 | (1,880,374,295) | (3,870,037,433.40) |
| Sale of Equipments | | - | - |
| **Net cash from investing activities** | | (1,880,374,295) | (3,870,037,433.40) |
| **Cash flows from financing activities** | | | |
| Long term borrowing | | - | - |
| Prepayment of Long term loan | | - | - |
| **Net cash used in financing activities** | | - | - |
| **Net cash Movements** | | (295,999,910) | (541,771,793) |
| **TSA Account to MOF** | | (140,651,381) | |
| **Cash and cash equivalents at beginning of period** | 17 | 1,614,122,043 | 2,155,893,836 |
| **Cash and cash equivalents at end of period** | | 1,177,470,752 | 1,614,122,043 |

The financial statements were authorised for issue by the Full Council on 7th January,2021 and were signed on its behalf by:

Name: **Theopister K. Mrango** Title: **DistrictTreasurer** Signature:______
Name: **Butamo N. Ndalahwa** Title: **Chairperson CMT** Signature:______
Name: **Ruth N. Mwelo** Title: **Secretary CMT** Signature:______

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KIBAHA DISTRICT COUNCIL
STATEMENT OF CHANGES IN NET ASSETS
FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2020

| | Accumulated surplus/deficit TZS | Minimum Compulsory Reserve | Total TZS |
|---|---|---|---|
| **Restated Balance at 30th June 2018** | | | |
| *Opening Balance* | 30,640,598,818 | 17,094,000 | 30,657,692,818 |
| **Balance** | 30,640,598,818 | 17,094,000 | 30,657,692,818 |
| Adjustment for Capital Grant that was wrongly deferred in previous | - | | - |
| Accumulated Employee benefits | (740,787,338) | | (740,787,338) |
| Surplus/Deficit for the year | 2,015,493,351 | - | 2,015,493,351 |
| Addition to Minimum Compulsory reserve | - | - | - |
| **Restated Balance at 30th June 2019** | 31,915,304,831 | 17,094,000 | 31,932,398,831 |
| Surplus for the year | 217,196,435 | | 217,196,435 |
| Transfer of Asset Ruwassa | (5,725,307,508) | | (5,725,307,508) |
| Transfer of Accumulated Depreciation to Ruwassa | 1,955,332,682 | | 1,955,332,682 |
| Adjustment of depreciation wrongly charged | - | | |
| Tranfer to Minimum Compulsory Reserve | - | - | - |
| **Balance at 30th June 2020** | 28,362,526,440 | 17,094,000 | 28,379,620,440 |

The financial statements were authorised for issue by the Full Council on 7th January,2021 and were signed on its behalf by:

Name: **Theopister K. Mrango** Title: **District Treasurer** Signature:______
Name: **Butamo N. Ndalahwa** Title: **Chairperson CMT** Signature:______
Name: **Ruth N. Mwelo** Title: **Secretary CMT** Signature:______

### 1.2 REPORT ON COMPLIANCE WITH LEGISLATIONS

**Compliance with the Public Procurement Act, 2011 (as amended in 2016)**

**Subject matter: Compliance audit on procurement of works, goods and services**

I performed compliance audit on procurement of works, goods and services of Kibaha District Council for the financial year 2019/20 as per stipulations of Public Procurement Act, 2011 and its Regulations of 2013 (as amended in 2016).

**Conclusion**
Based on the audit work performed, except for the matters described below, I state that, procurement of goods, works and services of Kibaha District Council is generally in compliance with the requirements of the Public Procurement Act, 2011 and its underlying Regulations of 2013 (as amended in 2016).

**Failure to implement Tanzania electronic Procurement System (TANePS)**
The Council did not make full utilization of TANePS for its procurement activities contrary to Section 9(1) (j) of the PPA, 2011 (as amended in 2016).

**Non-inclusion of procurements under force account in the Annual Procurement Plan and submission of the same to PPRA TZS 1,800,000,000**
The Council did not include procurement made for construction of District Hospital using force account in its Annual Procurement Plan and submit to PPRA contrary to the requirement of Sect.38 of PPA, 2011.

**Missing procurement documents and correspondences on force account worth TZS 301,638,030**
The Council made procurement through force account without maintaining proper documents and correspondences contrary to the requirement of Reg. 15(1) (b-d) and (6) of PPR, 2013.

Charles E. Kichere
**Controller and Auditor General**
**Dodoma, United Republic of Tanzania.**
**March, 2021**

*Controller and Auditor General* *AR/LG/VT.71-B4/2019/20*

216504302

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ligi Kuu Bara imenuka noti, waamuzi iongezeeni thamani

**KUNA** kila sababu wadau wa soka, mashabiki na klabu zote nchini kutembea kifua mbele wakilipongeza Shirikisho Soka Tanzania (TFF) na Bodi yake ya Ligi (TPLB), kwa kuweza kufanikisha kupatikana kwa wadhamini wa Ligi Kuu Bara ambao wameweka mabilioni ya fedha kwenye ligi hiyo inayoshika nafasi ya nane kwa ubora Afrika.

Kiasi cha fedha kilichowekwa na wadhamini wa ligi hiyo, ukianzia mdhamini wa haki za matangazo ya televisheni, Azam Media Ltd, matangazo ya redio, TBC, mdhamini mkuu, Benki ya NBC na wadhamini wenza Benki ya KCB, hakijawahi kutokea katika soka la nchi hii.

Kwa upande wa Azam Media Ltd, imeingia mkataba wa miaka 10 wenye thamani ya Sh. bilioni 225.6, ambazo ni zaidi ya Sh. bilioni 22.5 kwa kila mwaka kwa kipindi hicho, huku Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), lenyewe likiingia mkataba wa kurusha matangazo ya ligi hiyo kwa njia ya Redio kwa miaka 10 wenye thamani ya Sh. bilioni 3.54.

Mdhamini Mkuu Benki ya NBC, yenyewe imeingia makubaliano ya mkataba wa miaka mitatu na msimu huu wa kwanza benki hiyo itatoa kitita cha Sh. bilioni 2.5 kabla ya makato ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, VAT.

Kama hiyo haitoshi, bado TFF imeahidi kwamba muda si mrefu pengine wiki hii, ikaendelea kutangaza wadhamini wengine kwenye ligi hiyo ambayo msimu huu inashirikisha timu 16 tofauti na msimu uliopita ambao kulikuwa na timu 18.

Kwa hakika ni jambo la kupongezwa sana kwa TFF na TPLB, kwani udhamini kama huo haujawahi kutokea katika historia ya nchi yetu, hivyo hauna budi kulindwa kwa kila namna ili kuvutia wawekezaji wengi na wakubwa zaidi.

Hata hivyo, wakati huu ambao tayari ligi hiyo imeshaanza kwa kila klabu kushuka dimbani mara mbili, imeonyesha ushindani mkubwa kwa kila timu kupania kufanya vizuri zaidi ili kutwaa ubingwa ama kuendelea kusalia kwenye Ligi Kuu ili kunufaika na udhamini huo.

Hivyo, kikubwa ambacho tunataka kukiona sasa ni waamuzi kuhakikisha wanaiongezea ligi hiyo thamani hususan kwa kuchezesha kwa haki kwa kufuata sheria 17 za soka, ili kumpata bingwa aliyestahili atakayeiwakilisha vema nchi kwenye mashindano ya kimataifa, lakini kuvutia wawekezaji zaidi.

Tunatambua ubora wa ligi ndiyo kivutio kikubwa cha wawekezaji popote pale duniani, hivyo hatuwezi kuwa na ligi bora kama waamuzi hawatachezesha kwa haki na kufuata sheria 17 za soka zinazouongoza mchezo huu pendwa zaidi duniani.


Katika hilo, tunaikumbusha TFF na TPLB, kufungua makucha yake kwa mwamuzi yeyote yule atakayeonekana kufinyanga sheria 17 za soka kwa makusudi ama kwa mapenzi yake binafsi kwa klabu mojawapo au kwa dalili ya kupenyezewa rushwa.

Hivyo, Nipashe tukiwa wadau wakubwa wa michezo nchini, hatutasita kupaza sauti kila tunapoona dalili ya waamuzi kuchezesha kinyume cha kanuni 17 za soka zinazoongoza mchezo huo duniani, kwani tunataka kuona haki ikitendeka na ligi yetu kuzidi kuwa bora kutoka nafasi ya nane kwa ubora Afrika na kupanda juu zaidi.

Aidha, wachezaji pia wanapaswa kutambua mashabiki na wadau wa soka wanachotaka kukiona ni klabu zote kuonyesha ubora wa soka dimbani na si rafu mbaya za kukamiana ambazo zimeanza kujitokeza katika baadhi ya michezo iliyochezwa na kuhatarisha afya za wachezaji wenzao uwanjani.

Tunatambua soka la nguvu haliwezi kuepukwa katika ushindani mkubwa kama wa msimu huu, lakini zinapaswa kuwa nguvu zisizoumiza ama kuhatarisha afya za wengine, hivyo makocha na viongozi wa klabu hawana budi kulikemea hilo kwa kuhamasisha soka la kiungwana zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Benin imeacha somo ‘mapro’ Ligi Kuu Bara

Na Adam Fungamwango

**ACHANA** na matokeo ya jana ya ugenini kati ya Taifa Stars dhidi Benin, tunaangalia tuliyoyaona kwenye mechi ya kwanza iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Alhamisi iliyopita.

Stars ilipoteza kwa bao 1-0 kwenye mechi ya kuwania tiketi ya kufuzu kucheza Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar. Kwenye mechi hiyo Stars ilitengeneza nafasi nyingi, lakini kwa bahati mbaya haikuzitumia.

Sina nia ya kurudia kilichojitokeza kwenye mechi ile, lakini ukiiangalia timu ya Taifa ya Benin, tunapata kitu cha kujifunza kama Watanzania, kuanzia wachezaji, wanahabari na wanasiasa.

Kati ya wachezaji 24, waliochaguliwa ni saba tu ambao wanacheza soka la kulipwa Afrika, huku watatu tu wakiwa wanacheza Ligi Kuu nchini Benin. Tukianza na yule aliyefunga bao pekee, Steve Mounie, anaichezea klabu ya Stade Brestois ambayo ipo Ligi Kuu ya Ufaransa.

Kwa wenye kumbukumbu ni kwamba mchezaji huyo msimu wa 2017 mpaka 2020 alikuwa klabu ya Huddersfield Town na ameshacheza Ligi Kuu England mpaka timu hiyo inashuka daraja.

Golikipa wa timu hiyo ambaye kwa kiasi kikubwa aliinyima Tanzania bao, Saturnun Aliagbe, yeye anacheza Ligi Daraja la Pili Ufaransa kwenye klabu ya Valenciennes.

Nitataja baadhi ya wachezaji wa timu hiyo waliocheza mechi hiyo Dar na klabu zao kabla sijasema kile nilichokusudia ni Matheo Ahlinvi ambaye yuko Ligi Daraja la Pili Ufaransa kwenye klabu ya Nimes, Rodrgue Kossi, anaichezea Avranches pia ya huko, Oliver Verdon anaichezea klabu ya Ludogorets ya Ubelgiji, Tidjani Anaane, yeye yupo Menemenspor ya Uturuki na wengine wengi.

Sisemi hivyo kwa maana kuwa kwa sababu wanacheza Ulaya hatuwawezi, la hasha. Ninachotaka kusema hapa kuwa kumbe hata Watanzania wakiwa na nia, wanaweza kuwa na wachezaji wa kikosi cha timu ya taifa kikiwa na wachezaji wengi wanaocheza nje ya nchi. Kwa sasa tuna Mbwana Samatta, Simon Msuva na tumempata Dismas Novatus anayecheza soka la kulipwa nchini Israel.

Tunatakiwa sasa Watanzania kwenda huko. Kuwashawishi na kuwatengenezea mazingira wachezaji wetu kwenda nje ya nchi kusakata soka la kulipwa kwa maslahi ya nchi.

Hii ni tofauti na baadhi ya wadau wa michezo, wakiwamo wanasiasa, na wanahabari wanaolitaka Shirikisho la Soka nchini (TFF) kupunguza wachezaji wa kigeni ‘mapro’ ili kuwapa nafasi wachezaji wa Kitanzania, eti kwa ajili ya manufaa ya timu ya Taifa, Taifa Stars.

Wanadai wachezaji wengi wa kigeni wanaziba nafasi za wachezaji wa Kitanzania kuonekana au kuonyesha viwango na kuchaguliwa kwenye timu ya taifa.

Wanadhani mchezaji wa timu ya taifa ni lazima atoke Simba, Yanga ama Azam kwenye nchi hiyo hiyo husika. Kwenye kikosi cha Taifa Stars wapo wachezaji ambao hawajagusa Simba wala Yanga.

Pia tumeanza kuona baadhi ya wachezaji wakisajiliwa na timu hizo, baada ya kuitwa Stars kutoka kwenye klabu zingine. Mfano ni Kibu Denis alichaguliwa akitokea Mbeya City, sasa amesajiliwa na Simba, pia Israel Mwenda aliyekuwa KMC, sasa naye yupo Simba.

Kadhalika, mchezaji anaweza kwenda nje ya nchi bila kugusa timu hizo. Mfano ni Thomas Ulimwengu ambaye yupo TP Mazembe, pia Dismas ambaye alionekana akiwa na Biashara United. Hii inaonyesha kuwa Stars inaweza kuundwa bila kudai wachezaji wa kigeni kwenye klabu za Simba na Yanga wapunguzwe.

Ni kutowadekeza wachezaji wa Kitanzania kwa kuwatengezea urahisi wa kuwapunguza wageni, badala yake wapambane wenyewe waonyeshe viwango vyao, ambavyo ndivyo vitawafanya waonekane na kusajiliwa na klabu za nje, iwe hapa hapa Afrika au Ulaya.

Watoke kwenda nje ya nchi kama kina Msuva, Mbwana na Dismas ili Tanzania ikiita wachezaji, asilimia 70 wawe wanatoka nje, na timu za hapa ndani kuchangia asilimia 30 tu ya wachezaji.

Nadhani hata wimbo wa kusema wachezaji wa kigeni wanawabana Watanzania utaisha, pia hata msemo au dhana ya Usimba na Uyanga kwenye Stars nao hautokuwapo tena.

TANGAZO

# MWALIMU COMMERCIAL BANK PLC

MCB BANK BETTER TOGETHER

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

| WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2021 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-2021 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-2021 |
|---|---|---|
| **A. MALI:** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 216 | 494 |
| 2. Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 7,483 | 2,369 |
| 3. Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4. Salio katika Benki nyingine na Taasisi za fedha | 61 | 41 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | (32) | - |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 1,000 | 2,300 |
| 10. Uwekezaji katika Amana Nyingine | - | - |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 44,928 | 36,142 |
| 12. Mali Nyingine | 3,398 | 4,531 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14. Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 873 | 896 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **57,927** | **46,773** |
| **B. DHIMA:** | | |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| 18. Amana za Wateja | 39,165 | 27,832 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20. Amana Maalumu | - | - |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,048 | 880 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 116 | 90 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | 204 | 280 |
| 27. Dhima Nyingine | 1,305 | 1,637 |
| 28. Madeni | - | - |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | **41,838** | **30,719** |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI** | **16,089** | **16,054** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA:** | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 30,912 | 30,912 |
| 32. Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (18,507) | (18,507) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (1,316) | (1,351) |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji (Mtaji tangulizi) | 5,000 | 5,000 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **16,089** | **16,054** |
| **38. DHIMA ZISIZO DHAHIRI** | | |
| 39. Mikopo Chechefu | 500 | 346 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | (309) | (309) |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| - Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 27.8% | 34.0% |
| - Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 1.1% | 0.9% |
| - Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 113.9% | 129.0% |
| - Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 77.0% | 76.6% |
| - Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 79.3% | 82.0% |
| - Ongezeko la Amana | 40.7% | 16.0% |
| - Ongezeko la Mali | 23.8% | 8.0% |

| TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2021 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-2021 | Robo ya mwaka Linganishi 30-Sep-2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-2021 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Sep-2020 |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mapato ya Riba | 1,638 | 639 | 3,893 | 1,959 |
| 2. Gharama za Riba | 501 | 137 | 1,207 | 360 |
| **3. Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **1,137** | **502** | **2,686** | **1,599** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | - | (21) | (25) |
| 6. Mapata Yasiyo ya Riba: | 487 | 75 | 766 | 196 |
| 6.1 Faida (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za kigeni | - | - | 1 | 6 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 470 | 69 | 748 | 181 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 17 | 6 | 17 | 9 |
| 7. Gharama Zisizo za Riba | 1,589 | 1,731 | 4,789 | 4,900 |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 702 | 734 | 2,131 | 2,093 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 887 | 997 | 2,658 | 2,807 |
| **8. Faida (Hasara) ya Uendeshaji** | **35** | **(1,154)** | **(1,316)** | **(3,080)** |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| **10. Faida (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **35** | **(1,154)** | **(1,316)** | **(3,080)** |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | | - | | - |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **35** | **(1,154)** | **(1,316)** | **(3,080)** |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 55 | 62 | 55 | 62 |
| 14. Mapato kwa Hisa | 1 | -19 | -21 | -50 |
| 15. Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| - Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | *0.1%* | *-3.7%* | *-2.8%* | *-11.0%* |
| - Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | *0.2%* | *-8.0%* | *-8.1%* | *-21.0%* |
| - Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | *97.8%* | *300.0%* | *138.7%* | *273.0%* |
| - Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | *2.5%* | *3.3%* | *5.8%* | *8.0%* |

| TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2021 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Mtaji wa Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Mtaji tangulizi | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (18,507) | - | - | 12,405 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (1,316) | - | - | (1,315) |
| Mtaji tangulizi | - | - | - | 5,000 | 5,000 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(19,823)** | **-** | **5,000** | **16,090** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (14,445) | - | - | 16,467 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (4,062) | - | - | (4,062) |
| Mtaji tangulizi | - | - | - | 5,000 | 5,000 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(18,507)** | **-** | **5,000** | **17,405** |

| TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2021 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-2021 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Sep-2020 |
|---|---|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato (Hasara) Halisi | 35 | (403) | (1,316) | (1,927) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| - Hasara katika Mali | 326 | 343 | 1,015 | 614 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (7,486) | (5,279) | (18,531) | 805 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 8,133 | 6,996 | 20,640 | (2,147) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (215) | 296 | (161) | (16) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 893 | 100 | 191 | 991 |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **1,686** | **2,053** | **1,838** | **(1,680)** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | - | - |
| - Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Mali za Kudumu | (30) | (120) | (150) | (12) |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(30)** | **(120)** | **(150)** | **(12)** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | - | - |
| - Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| - Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| - Mengineyo (Mtaji tangulizi) | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | - | - |
| - Ongezeko / Punguzo Halisi katika Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu | 1,656 | 1,933 | 1,688 | (1,692) |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 4,891 | 2,958 | 4,485 | 4,274 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 6,547 | 4,891 | 6,173 | 2,582 |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2021**

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha za robo, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Richard L. Makungwa (Ofisa Mtendaji Mkuu) | ........................ (Imesainiwa) | 8 Octoba 2021 |
| Selemani Kijori (Mkuu wa Fedha) | ........................ (Imesainiwa) | 8 Octoba 2021 |
| Patrick Mashalla (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | ........................ (Imesainiwa) | 8 Octoba 2021 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya sheria ya benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1/ Francis Ramadhani (Mwenyekiti) | ........................ (Imesainiwa) | 8 Octoba 2021 |
| 2/ Enna Victor Mwakipesile (Mkurugenzi) | ........................ (Imesainiwa) | 8 Octoba 2021 |

## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES MADE UNDER REGULATION 11

| S/N. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| 1 | **Current Accounts** | |
| | (a) Required minimum opening balance | TZS 50,000 |
| | (b) Monthly service fee (breakdown per customer type) | TZS 7,500 |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS 2,500 for amounts less than 5Mil otherwise 0.1% max TZS 100,000 |
| | (d) Fees per ATM withdrawal | TZS 1,300 |
| | (e) ATM mini statement | TZS 300 |
| | (f) Interim statement per page | TZS 1,500 |
| | (g) Periodic scheduled statement | 0 |
| | (h) Cheque book | TZS 500 per leaf |
| | (i) Dishonoured cheque | TZS 100,000 |
| | (j) Special clearance | n/a |
| | (k) Counter cheque | TZS 6,000 |
| | (l) Stop payment | TZS 40,000 |
| | (m) Standing order (Same bank) | Free |
| | (n) Balance enquiry | TZS 300 |
| | (o) New ATM card issuance | TZS 10,000 |
| | (p) ATM card renewal or replacement (indicate costs for different card types) | TZS 10,000 |
| | (q) Overdrawn account interest charge | 20% |
| | (r) Unarranged overdraft | 20% |
| | (s) Interbank transfer | TZS 10,000 |
| | (t) Bill payments through ATM | n/a |
| | (u) Deposit fee | 0 |
| | (v) Other (please specify) | n/a |
| 2 | **Savings Accounts (Disclose for product specific types)** | |
| | (a) Required minimum opening balance | TZS 5,000 |
| | (b) Monthly service fee | TZS 0 |
| | (c) Interim statement | TZS 1,500 |
| | (d) Account closure | TZS 20,000 |
| 3 | **Electronic Banking** | |
| | (a) Internet banking monthly fee | n/a |
| | (b) Internet transfers | n/a |
| | (c) SMS banking | TZS 1700 |
| | (d) Other | n/a |
| 4 | **Foreign Exchange Transaction** | |
| | (a) Purchase/sale of TCs transactions over the | n/a |
| | (b) Purchase of foreign cheque | n/a |
| | (c) Sale/purchase of cash passport | n/a |
| | (d) Telegraphic transfer | n/a |
| | (e) Telex/SWIFT | n/a |
| | (f) Tranfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank) | 0 |
| 5 | **Personal Loans** | |
| | (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | 1.30% p.a |
| | (i) Personal loans | 16% |
| | (ii) Overdrafts | 20% |
| | (iii) Mortgage finance | n/a |
| | (iv) Asset finance | n/a |
| | (b) Unpaid loan instalment | 20% |
| | (d) Valuation fees | n/a |
| | (e) Other | n/a |

**Deposit Rates**

| Fixed Deposit - TZS | 3 Months | 6 Months | 12 Months |
|---|---|---|---|
| 1 - 2 Mln | 1.5% | 2.0% | 2.5% |
| 2 - 10Mln | 2.0% | 2.5% | 3.0% |
| 10 - 50 Mln | 2.5% | 3.0% | 3.5% |
| 50 - 100 Mln | 3.0% | 3.5% | 4.0% |
| 100 - 300 Mln | 3.5% | 4.0% | 4.5% |
| 300 - 500 Mln | 4.0% | 4.5% | 5.0% |
| 500m - 1Bln | 4.5% | 5.0% | 5.5% |
| Above 1 Bln | Contact Treasury | | |

| Savings Account - TZS | Accrue on Daily Cleared balance paid Monthly |
|---|---|
| 0- 50k | 0.5% |
| 50k - 1mln | 1.0% |
| 1 - 10mln | 1.5% |
| 10 - 100mln | 2.0% |
| Over 1mln | 2.5% |

**Base Lending Rates**

| | Loan Type | Base rate | |
|---|---|---|---|
| 1 | Short term (up to 1year) | 19.5% | +/-4.5% |
| 2 | Medium term (2-4 years) | 21.5% | +/-1.5% |
| 4 | Term loans (over 5 years) | 19.0% | +/-4.0% |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Richard L. Makungwa | Chief Executive Officer | | 8 October 2021 |
| 2 | Leticia Ndongole | Head of Business Development & Marketing | | 8 October 2021 |
| 3 | Selemani Kijori | Head of Finance | | 8 October 2021 |

216504002

# W/biashara kukamatwa tuhuma deni la benki

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania (Idara ya Biashara) jijini Dar es Salaam imeagiza kukamatwa kwa wadeni watatu wa Benki ya Exim Tanzania kwa kushindwa kutekeleza hukumu ya kulipa deni lenye thamani ya Sh. milioni 674.4 na zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 2.

Kwa mujibu wa hati ya kukamatwa kwa wadeni hao iliyotolewa na mahakama hiyo katika kesi ya kibiashara nambari 95 ya mwaka 2015, Kamanda wa Polisi mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Justine Masejo, ameagizwa kuwakamata wadeni hao watatu ambao ni Chimanbhai Marghabai Patel, Pratik Chimanbhai Patel na Sonia Pratik Patel. Kwa mujibu wa hati hiyo iliyosainiwa Septemba 13, 2021 na Naibu Msajili wa Mahakama hiyo, watatu hao walihukumiwa katika kesi hiyo Septemba 16, 2016, kuilipa Benki ya Exim Tanzania Limited Sh.

674,440,547.55 na Dola za Kimarekani 2,024,094.14 pamoja na riba na gharama ya kesi hiyo.

Hata hivyo licha ya hukumu hiyo kutolewa, fedha hizo hazijalipwa kwa benki hiyo.

Kufuatia ucheleweshaji huo, ndipo mahakama hiyo iliamuru kukamatwa kwa watatu hao.

"Unaagizwa kurudisha hati hii mnamo tarehe 27 Oktoba, 2021, sambamba na uthibitisho unaoonyesha siku na namna ambavyo hati hii imetekelezwa au sababu zilizosababisha kushindwa kutekelezwa kwake," ilisomeka sehemu ya hati hiyo.



Mkurugenzi Mkuu na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bank of Africa, Adam Mihayo (katikati), akifurahi na baadhi ya wateja wa benki hiyo tawi la Oysterbay jijini Dar es Salaam wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jafo apiga marufuku pastiki laini

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amepiga marufuku matumizi ya plastiki laini kwenye mifuniko ya chupa za vinywaji baridi hasa zile za maji na mirija ya plastiki baada ya miezi sita kuanzia leo.

Alitangaza marufuku hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema plastiki hizo ni hatari kwa mazingira kwa sababu imethibitika kuwa hazirejelezeki na zimetapakaa maeneo mengi, hivyo kuhatarisha maisha ya binadamu na viumbe wengine kama ndege wanyama na mimea.

"Kutokana na changamoto hiyo tumeona tuchukue hatua kali na tumetoa miezi sita kuanzia tarehe 11 mwezi huu na baada ya miezi sita hatutarajii kuona vikitengenezwa tena na tunaagiza kwa wazalishaji wa vinywaji baridi wasiweke plastiki laini kwenye chupa na hata zile zinazotoka nje ya nchi hazitaruhusiwa kuingia," alisema.

Alisema jukumu la wizara yake ni kulinda mazingira kwa namna yoyote Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Ndilo limepewa nguvu ya kusimamia mazingira na kuna maelekezo mbalimbali ya serikali ambayo yalitolewa nyuma kama kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya rambo ambayo ilifanikiwa kwa kiasi kikubwa.

"Tuliwahi kutoa maelekezo ya kuzuia mifuko ya rambo tukaweka katazo na tulipata mafanikio makubwa sana sasa hivi kumetokea changamoto kubwa katika vinywaji hasa maji nako lazima tuchukue hatua zile zile kulinda mazingira yetu na tutafanikiwa," alisema Jafo.

Vilevile, alipiga marufuku uzalishaji na matumizi ya mirija ya plastiki inayotumika kwenye vinywaji mbalimbali ambayo nayo huwa hairejelezwi hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa kuharibu mazingira.

"Ile mirija huwa hairejelezwi na hakuna namna ya kuirejeleza na hata wanaookota plastiki huwa hawaiokokoti sasa matokeo yake imejaa barabarani na baadhi ya nchi wameshapiga marufuku wao wanazalisha wanatuuzia sisi tu wakati wao hawaitumii hivyo nasisi tunakataa kuizalisha na kuitumia," alisema.

Alisema bidhaa ambazo zimezalishwa kabla ya katazo hilo na ambazo muda wake wa matumizi haujaisha zitaendelea kubaki sokoni na wahusika wasisumbuliwe hadi pale muda wake wa matumizi utakapofika.

Alisema bidhaa zote zote za vinywaji baridi zenye plastiki laini kwenye mifuniko zitakazozalishwa miezi sita ijayo baada ya katazo hilo linaloanzia leo hazitaruhusiwa kuingia sokoni.

# Mkurugenzi CRDB apewa tuzo

**Na Faustine Feliciane**

MKURUGENZI Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, amechaguliwa kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu Bora wa mwaka 2021 katika Tuzo ya Uongozi Bora katika mashirika.

Nsekela alipokea tuzo hiyo kwenye hafla ya mwisho ya orodha ya watendaji bora 100 wa Tanzania mwishoni mwa wiki katika hafla ya kila mwaka.

Kwa mujibu wa waandaaji wa tuzo hizo, lengo ni kutambua na kusherehekea mafanikio ya mtu binafsi na mashirika. Tuzo hizo ziliandaliwa na Taasisi ya 'Eastern Star Consulting' kwa lengo la kuhamasisha maofisa kuanzia ngazi ya chini kwenye mashirika makubwa.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, alielezea kujitolea kwa serikali katika kuwezesha uwekezaji na biashara, akisema itaongeza ujasiri wa wafanyabiashara wa Tanzania kushindana katika soko la kimataifa.

Alisema serikali inafanyika kazi baadhi ya sera ili kuboresha urahisi wa kufanya biashara ikiwa ni pamoja na kushirikisha sekta binafsi na kupunguza uwepo wa serikali katika biashara hizo.

Alisema kulikuwa na pengo kubwa la ustadi kati ya wahitimu wa Kitanzania huku waajiri wakilaumu taasisi za juu za elimu kwa kuzalisha wataalam wasiokidhi vigezo, huku wakisahau kuwa mafunzo kazini yanamjenga na kupanua uwelewa zaidi kwa mfanyakazi.

Alisema tuzo zilizotolewa zitaongeza juhudi kwa maofisa na watendaji wa mashirika katika maeneo yao ya kazi kwa kuwa wataona juhudi na maarifa kwa kuwa yanathaminiwa kwa tuzo kama hizo.

Wengine waliopata tuzo ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya TPB, Sabasaba Moshingi ambaye aliibuka wa pili kwa kura akifuatiwa na Jared Awando wa Shirika binafsi la Bima la ICEA.

Aidha, kipengele kingine katika tuzo hizo, Friedrick Nshekanabo kutoka CRDB alichaguliwa kuwa Ofisa Mwendeshaji Mkuu Bora, huku Christina Manyenye kutoka KCB Benki aliibuka mshindi wa Ofisa Biashara Mkuu.

Katika hotuba yake wakati akipokea tuzo hiyo Ofisa Mtendaji Mkuu Bora, Nsekela alisema tuzo hiyo si kwa juhudi zake peke yake bali pia imechangiwa na wafanyakazi wenzake wa CRDB.

"Haya ni matokeo ya kufanya kazi kama timu, lakini upendo na urafiki baina yetu... tuzo hii naitoa kwa familia yangu, mke na watoto wangu kwa kunipa utulivu, bila utulivu kichwani ni ngumu kufanya vizuri," alisema Nsekela.

# UBA kusogezea wateja huduma

**Na Enock Charles**

BENKI ya UBA Tanzania imewahakikishia wateja wake na umma kwa ujumla kuwa itaendelea kuwapa huduma bora.

Imesema hayo katika maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja kwa lengo la kupata mrejesho wa kutoka kwa wateja na kuwapa huduma bora kila siku na hasa kipindi hiki cha janga la UVIKO-19.

Mwendashaji Mkuu UBA Tanzania, Flavia Kiyanga, aliwapongeza wateja wa benki hiyo kwa kuwa wateja wazuri jambo ambalo linawapa UBA Benki fursa ya kuwahudumia.

Flavia alisema: 'Tukiwa tunaendelea ushirikiano wetu na wateja, Benki ya UBA imekuwa ikiwekeza kupanua wigo wake kwa lengo la kuleta huduma zake karibu na wateja kwa kufungua tawi la Mwanza na Kijitonyama ili kukidhi matakwa na malengo ya wateja kwa sababu lengo letu ni moja tu kutoa huduma bora.'

'Tutaendelea kuwa waaminifu kwa wateja wetu, tunahaidi kuendelea kuwa kwenye moyo na akili zao huku tukizidi kupanua wingo wa matawi yetu pamoja na kuwa na huduma bunifu na kuongeza ufanisi kwenye huduma za kidigitali ili kuendana na madaliko ya teknolojia ili wateja wetu waendelee kupata huduma pamoja na kufanya miamala yao muda wowote na sehemu yeyote.

Mkuu wa Idara ya Masoko wa Benki ya UBA Tanzania, Brendasia Kileo, alisema: "Benki yetu inafanya kazi kwa kuzingatia ubora wa huduma kwa wateja, mteja kwetu ni muhimu sana. Tunatoa pia mafunzo kwa wafanyakazi wetu na kuwaelewesha umuhimu wa kutoa huduma bora."

Kileo alisema benki hiyo imewekeza vema katika teknolojia ya mitandao ambayo ni salama na haraka zaidi.

# Wanawake wapigiwa debe wawe viongozi

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WANANCHI wametakiwa kushirikiana katika kuwainua wanawake, ili kuhakikisha wanakuwa viongozi kuanzia ngazi ya jamii hadi Taifa.

Akizungumza na wananchi wa shehia ya Tumbe Magharibi, Mkurugenzi wa Jumuiya ya PEGAO Pemba, Hafidh Abdi Said, alisema, wanawake wana uwezo wa kuongoza na kuleta mabadiliko ya haraka, hivyo ni vyema jamii ikampa ushirikiano katika kuusaka uongozi.

Alisema, katika jamii kuna vikundi na jumuiya mbalimbali zinazoanzishwa kwa ajili ya kuleta maendeleo, ingawa kinachomshangaza ni kuona kuwa wanawake hunyimwa hata nafasi hizo, jambo ambalo sio sahihi kwani wanawafanya waendelee kubaki nyuma kila uchao.

"Tumekuwa tukiwanyima wanawake nafasi hata hizi za jumuiya ndogo ndogo tunazoziunda kwenye jamii, sasa tunataka tumwinue mwanamke ili na yeye awe kiongozi kwani wanaweza kuleta mabadiliko makubwa, alisema mkurugenzi huyo.

Aidha, aliwataka wanaume kuwaunga mkono kinamama wanaotia nia ya kugombea uongozi, kwani kila mmoja anamtegemea mwenzake katika harakati mbalimbali za kijamii, kisiasa na kiuchumi katika kufikia malengo.

Akiwasilisha mada katika mkutano huo, Mudathir Sharif Khamis, alisema, kila mmoja yuko sawa mbele ya sheria, hivyo si vyema kumnyima mwanamke kugombea uongozi kwa kisingizio cha kuwa yeye ni mama wa nyumbani.

"Kinababa tusiwabane wanawake, wapo viongozi wanawake ambao wanaongoza na wanaleta mabadiliko makubwa katika jamii yetu," alisema Mudathir.

Naye mwasilishaji, Hadia Sultan Hamad, alieleza, kuna baadhi ya wanajamii humkwamisha mwanamke katika kugombea nafasi hizo kwa kisingizio cha dini, jambo ambalo sio sahihi kwani waliwahi kuwapo wanawake wa kiislamu ambao walikuwa wakisimamia mambo mbalimbali katika jamii zao.

"Tuwaelimishe watoto wetu wa kike tangu wakiwa shule na kuwaelekeza kwamba na wao wanayo haki ya kugombea uongozi, ili watakapofikia muda wasione ajabu badala yake wawe mstari wa mbele katika hili," alisema.

Maryam Hemed Said, mkazi wa Tumbe, alieleza kuwa wanawake ambao ni viongozi wametoa mchango mkubwa katika jamii na juhudi mbalimbali zinaonekana katika kuliletea Taifa maendeleo.

Akichangia, Ali Mohamed Bakar alisema wanawake wanashindwa kufikia uongozi kutokana na mifumo ya kiutawala iliyopo katika vyama, kutokana na kuwawekea vizingiti.

"Wakati mwingine utaona kwamba mwanamke anapata nafasi ya pili katika watu tisa waliogombea na wote huwa ni wanaume... kwanini tusimpe kipaombele kwa kwa ujasiri wake aliouonyesha, vyama vibadili mifumo yao na vimpe nafasi mwanamke," alisema.

Kwa upande wao wananchi wengine walisema kuwa kumekuwa na viongozi kwenye majimbo ambao huwashawishi wapigakura wasimpe mwanamke na kuwapandikiza chuki zisizo na sababu, jambo ambalo linawaumiza sana wanaogombea.



Mkurugenzi Mkuu wa SNV wa Dunia, Megan Ritchie (kulia), akigonganisha glasi na Mkurugenzi wa Shirika hilo nchini, Duncan Rhind, Balozi wa Uholanzi nchini, Wiebe de Boer, Msajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Vickness Mayao (wapili kushoto) na Mkurugenzi wa Afya, Ustawi wa Jamii na Idara ya Huduma za Lishe, Dk. Ntuli Kapologwe (kushoto), katika hafla ya kuadhimisha miaka 50 ya Shirika la SNV Tanzania tangu lianze kufanya kazi nchini iliyofanyika jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaharakati wataka jamii kumtua mzigo mtoto wa kike

**Na Yasmine Protace**

KATIKA kuelekea maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike, wadau wa semina za Jinsia na Maendeleo (GDSS,) wamesema jamii inatakiwa kupatiwa elimu, ili kumtua mzigo mtoto wa kike.

Wadau hao wamebainisha baadhi ya changamoto ambazo anapitia mtoto wa kike kuwa ni kukosa elimu, kufanyishwa kazi, kuachiwa majukumu ya kifamilia.

Washiriki wa GDSS, waliyasema hayo kwa nyakati tofauti walipokuwa wakijadili kueleke maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike kuhusu walivyojipanga kwa changamoto hizo.

Zahara Omary, alisema kuwa kuna baadhi ya wazazi ambao huwanyima haki watoto wao.

"Unakuta mtoto anatakiwa kucheza na watoto wenzake, lakini unakuta familia ya huyo mtoto wa kike inamzui kutoka nje kucheza na wenzake," alisema.

Aliongeza kuwa kuna kesi iliishafikishwa ofisini kwake ambapo mtoto wa kike ambaye anatakiwa kusoma hakupelekwa kusoma na akaletwa Tanzania akitokea Kenya kuja kufanya kazi za ndani.

Alisema mtoto huyo alikutana na manyanyaso ambapo utaratibu ulifanywa na akarudishwa kwao.

Rehemsa Mwinyi, alisema kuwa baadhi ya watoto wa kike wamekuwa wakipitia changamoto nyingi na kwamba hali hiyo isipochukuliwa hatua inaweza kusababisha watoto hao kutofikia malengo yao.

"Kumekuwa na changamoto kubwa ambazo baadhi ya watoto wamekuwa wakizipitia, hivyo jamii inatakiwa kupewa elimu ili waweze kujua haki za mtoto wa kike," alisema.

Aman Giba, alisema mtoto wa kike ana haki sawa na mtoto wa kiume, lakini baadhi ya jamii zimekuwa zikimwona mtoto wa kike hana haki, hivyo kumpa mzigo mkubwa wa majukumu ya kifamilia.

Pia aliitaka sheria ziwabane watu wanaowadhalilisha watoto wa kike kupitia mitandao ya kijamii.

# Shule Dar yapigwa jeki ya madawati

**Na Beatrice Moses**

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Tuangoma wilayani Temeke, mkoani Dar es Salaam wameondolewa adha ya uhaba wa madawati, hivyo kusomea katika mazingira bora.

Wamepataa unafuu huo baada ya Benki ya Stanbic Tanzania kutoa madawati 100 yenye thamani ya milioni 9 kwa shule hiyo.

Msaada huo ni ikiwa sehemu ya kampeni inayoendelea ya benki hiyo ya 'Stanbic Madawati Inititaive' ambayo inakusudia kuboresha mazingira ya kujifunzia na kuchochea maendeleo ya elimu nchini.

Madawati hayo yalikabidhiwa na Mkuu wa Kitengo cha Wateja wa Rejareja wa benki hiyo, Omari Mtiga, kwa Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, katika hafla iliyofanyika kwenye eneo la shule hiyo jana.

Mtiga alisema benki hiyo imejikita kuboresha mazingira ya kujifunzia katika shule tofauti nchini Tanzania, kupitia kampeni ya Stanbic Madawati Initiative, ambayo inakusudia kuchangia madawati 1,000 nchini kwa mwaka huu. "Tunaamini kwamba ndoto zote zinawezakana ikiwa zitapewa msaada unaohitajika. Mchango huu utasaidia kuboresha mazingira ya kujifunzia na kuchochea ufaulu wa wanafunzi wa Tuangoma." Aliongeza kuwa kampuni hiyo hivi karibuni ilitoa msaada kama huo kwa Shule ya Sekondari ya Mbabala huko Dodoma na ina nia ya kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali kwa kutoa madawati kwa shule katika maeneo mengine ya nchi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegola, alipongeza juhudi za Benki ya Stanbic katika kusaidia serikali kuboresha elimu na akawataka wawekezaji wengine kuiga hatua hiyo.

Alitoa wito kwa uongozi wa shule kuhakikisha kwamba madawati yanatumiwa vizuri, ili waweze kufaidika wanafunzi wengi iwezekanavyo, na pia amewataka wanafunzi kufanya kazi kwa bidii ili kuboresha ufaulu wa shule.

# Wanachama PSSSF waridhishwa huduma

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

WANACHAMA wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Watumishi wa Umma (PSSSF) mkoani Tanga wakeeleza kuridhishwa na huduma wanazopatiwa na kwamba wanahudumiwa haraka na kuzingatia weledi.

Walibainisha hayo wakati wa kusherehekea Wiki ya Huduma kwa Wateja mwishoni mwa wiki.

Akizungumza ka niaba ya wastaafu waliokwenda kupatiwa huduma katika Ofisi za PSSSF Tanga, mwalimu mstaafu, Valentine Ngoiya Adriano, alisema huduma za ofisi ya PSSSF Tanga ni zenye kuzingatia weledi na uharaka ambayo inatusaidia kupata majibu ya madai yao kwa wakati.

Akielezea ni nini anachotegemea kama mteja na mwanachama wa PSSSF, Mwalimu Valentino alisema baada ya kutumikia serikali kwa kipindi kirefu anategemea kupata huduma kama mteja anayethaminiwa kwa kujali utumishi uliotukuta ambao ametumikia katika Taifa.

Alitoa rai kwa uongozi wa Mfuko wa PSSSF kutoa elimu juu ya mafao ili wastaafu waweze kuwa na matumizi sahihi ya kiinua mgongo ambacho wamepata katika uzee wao.

"Wastaafu wengi hupoteza pesa ambazo wamepata kama kiinua mgongo kwa sababu ya kuingia katika biashara ambazo kimsingi haziendani na umri wao na hivyo kupoteza pesa na matokea yake kuishi maisha ya uzee ambayo hayana staha," alisema.

Katika salamu zake kwenye kilele cha Wiki ya Huduma kwa Wateja ambayo ilianza Oktoba 4, 2021 na kufikia kilele Oktoba 8, 2021 Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko huo, Hosea Kashimba, alisema PSSSF inawahakikishia wanachama wake na jamii kwa ujumla kuwa itaendelea kutoka huduma bora wakati wote.

"Ujumbe wa Wiki ya Huduma kwa Wateja ni nguvu ya huduma yaani Power of Service, sisi tutajikita katika kuonyesha ni namna gani tutajenga imaani kwa wateja wetu kwa kutumia teknolojia tuliyonayo kumaliza kero zao," alisema Kashimba na kuongeza:

"Kutumia mtandao wa ofisi zetu kupunguza muda ambao mwanachama wetu angefika kutatuliwa matatizo yake, kutasaidia sana kupunguza kero kwa wanachama wetu."

Aliahidi kuendelea kwa ukarimu wa wafanyakazi wa PSSSF kuwa watawahudumia wanachama vizuri wafikapo kwenye ofisi za mfuko na watatoka wameridhika.

Aliwakumbusha wafanyakazi wa mfuko kuendelea kutumia lugha nzuri wanapowahudumia wanachama, kutanguliza upendo na uwajibikaji ili mwanachama anapotoka ofisini aridhike kweli kahudumiwa.

Akizungumza na wanachama waliokwenda kupata huduma katika ofisi za PSSSF Tanga, Meneja wa Huduma kwa Wateja, Laila Maghimbi, alisema katika Wiki ya Hduma kwa Wateja PSSSF inasherehekea kazi kubwa inayofanywa na watumishi wa PSSSF ya kuangalia na kulinda maslahi ya wanachama.

# GGML yaikabidhi Polisi jengo la ofisi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA jitihada za kuboresha mazingira bora ya kufanyia kazi kwa taasisi mbalimbali za serikali, Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imekabidhi jengo jipya kwa ajili ya kusaidia shughuli mbalimbali za Jeshi la Polisi mkoani Geita.

Akizungumzia ufadhili wa ujenzi wa jengo hilo lenye ofisi tatu juzi mkoani Geita, Makamu wa Rais wa GGML anayeshughulikia miradi endelevu, Simon Shayo, alisema kuwa pamoja na kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo mkoani Geita na Tanzania kwa ujumla, usalama wa miradi hiyo bado ni jambo la msingi ambalo muda wote limekuwa likisimamiwa na Jeshi la Polisi.

"Jeshi la Polisi ni wadau wetu muhimu katika shughuli mbalimbali tunazozifanya. Tunashirikiana nao katika maeneo mengi, hususani ulinzi mgodini na ulinzi shirikishi kwenye mitaa na vijiji vinavyotuzunguka.

"Tulipoona uhitaji wa ofisi kama mojawapo ya vikwazo vya utekelezaji wa majukumu ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Geita tuliguswa na tukaanza mara moja jitihada za kuwapatia jengo hili ambalo litasaidia maofisa wa jeshi hili kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na kupunguza msongamano, hasa katika kipindi hiki cha ugonjwa wa UVIKO-19 ambao unaweza kuepukwa kwa kupunguza misongamano kwenye maeneo yetu ya kazi," alisema Shayo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Geita, Hendry Mwaibambe, aliishukuru GGML kwa ufadhili huo kwani utasaidia zaidi kuongeza ufanisi wa shughuli za ulinzi na usalama mkoani Geita.

"Kwa niaba ya Inspekta Jenerali wa Polisi nchini, nawapongeza kwa dhati kabisa kampuni ya GGML kwa kuwa wadau wetu muhimu wa maendeleo, ikiwa ni pamoja na kutusaidia ujenzi wa ofisi hii ya kisasa yenye mahitaji yote muhimu.

"Tunatambua pia mchango wao mwingine wa kutupatia gari mapema mwaka huu. GGML wamekuwa pia wakitufanyia matengenezo, kutupatia magurudumu mapya na mafuta kila mara tunapohitaji msaada huo.

"Tunawahakikishia kuwa tutaendelea kusimamia ulinzi na usalama katika mkoa huu ili wananchi wote, ikiwa ni pamoja na GGML wenyewe waweze kufanya shughuli zao kwa amani, usalama na tija kwa ajili ya uchumi na maendeleo ya nchi yetu," alisema Kamanda Mwaibambe.



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Hosea Kashimba (kulia), akimsikiliza mmoja wa wananchama wa mfuko huo katika kilele cha Wiki ya Huduma kwa Wateja iliyofanyika Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SGA yaanzisha kituo cha kisasa

**Na Christina Mwakangale**

KAMPUNI ya ulinzi ya SGA imezindua kituo cha kisasa cha mawasiliano, ikiwa sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, uliofanyika katika makao makuu ya kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa SGA Tanzania, Eric Sambu, alisema kituo hicho kipya kitatoa huduma saa 24.

Alisema kampuni hiyo inajivunia katika kutoa huduma bora na za viwango vya juu kwa sababu imewekeza katika mitambo ya kisasa na mafunzo kwa wafanyakazi na yote haya yatakuwa na ufanisi ikiwa mawasiliano kati ya kampuni na wateja yatafanyika kwa haraka zaidi.

"Tuna imani na wafanyakazi wetu na tumewekeza vilivyo katika kuwawezesha ili waiwakilishe kampuni vizuri kwa fahari. Tunaamini kituo hiki kitasababisha wafanye kazi kwa weledi zaidi na kwa kujiamini," alisema.

Alisema timu za dharura za SGA zina mawasiliano ya moja kwa moja na chumba cha mawasiliano mara tu inapobonyezwa alamu na wafanyakazi wa kituo cha mawasiliano wanaweza kuona maeneo walipo kwa kutumia mitambo maalumu iliyounganishwa kwenye ramani za google na kuwaongoza katika eneo liliporipotiwa tukio. Ishara fulani huonekana kwenye ramani kwani gari lilikloko karibu pia hupewa taarifa kuwahi katika eneo la tukio.

"Nguvu yetu ipo katika uwezo wa timu zetu kuwahi katika eneo la tukio huku wakiwa na vifaa vya kutosha, mafunzo na silaha," alisema Sambu.

Meneja Huduma kwa Wateja wa SGA Tanzania, Aikande Makere, alisema wateja wategemee huduma bora zaidi baada ya uzinduzi wa kituo hicho cha kisasa.

Naye Meneja Masoko wa SGA Tanzania, Faustina Shoo, alisema kampuni hiyo itatoa punguzo la asilimia 25 kwa bei ya huduma za dharura kwa miezi mitatu ijayo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja.

# Nipashe Spotika




WACHEZAJI 7 WENYE MABAO MENGI DHIDI YA TIMU 6 ZA EPL UK. 12 - 13




SOLSKJAER

# MAKOCHA WA4 WALIOKALIA KUTI KAVU

**LONDON,** England

MAKOCHA wanakuwa wa kwanza kukosolewa pale timu inapokuwa na matokeo mabaya uwanjani. Kocha ni sura ya klabu, kwa hiyo yeye ndiye mtu wa kwanza kushughulikia mazuri na mabaya.

Kocha anapaswa kushughulikia athari na hasara pia. Katika klabu kubwa za juu shinikizo linakuwa ni kubwa kila wakati.

Kwa hivyo, makocha wanatembea njia nyembamba, na wanapaswa kuwa waangalifu na kile wanachosema na kuhakikisha kuwa timu inafanya vizuri katika kila mchezo unaokuja.

Makala haya yanawaangalia makocha wanne ambao wamekalia kuti kavu kwa sasa, shuka nayo sasa...

**#4. MIKEL ARTETA (ARSENAL)**

Mtazamaji wa kawaida wa mpira wa miguu anaweza kudhani kwamba Mikel Arteta yuko chini ya shinikizo kila wakati. Hiyo ni kwa sababu wakati wake pale Arsenal unaendelea kuwa mgumu kwake.

Arteta alihusishwa sana na jukumu la usimamizi wa klabu hiyo baada ya Arsene Wenger kuachia ngazi. Lakini klabu ikamteua Unai Emery, na Arteta alijiunga na Manchester City kama msaidizi wa Pep Guardiola. Arteta alifurahia wakati mzuri kule City, ambapo alisifiwa sana kwa michango yake.

Inaeleweka, mashabiki wa Arsenal walifurahi baada ya kuteuliwa kwake mwaka 2019. Aliongoza klabu kutwaa FA na Ngao ya Jamii mwaka 2020. Lakini tangu wakati huo, mambo hayajaenda kulingana na mpango.

Arsenal walikuwa wabaya msimu uliopita, wakimaliza nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu. Licha ya kutumia fedha nyingi msimu huu wa majira ya joto, 'Washikabunduki' hao kwa sasa wako katika nafasi ya tisa kwenye ligi.

**#3. NUNO ESPIRITO SANTO (TOTTENHAM HOTSPUR)**

Tottenham Hotspur msimu huu wa majira ya joto, walikuwa kwenye hekaheka za kutafuta kocha mpya. Walitajwa Antonio Conte, Paulo Fonseca, Gennaro Gattuso na Hansi Flick, lakini mwishowe wakamteua Nuno Espirito Santo kuwa kocha wao mpya.

Santo aliondoka Wolverhampton Wanderers msimu wa majira ya joto. Chini yake, Wolves ilikuwa imeinuka na kuwa moja ya timu yenye ushindani mkubwa kwenye Ligi Kuu. Lakini wasiwasi uliibuka juu ya mtindo wao wa uchezaji, na Santo alipendelea zaidi mchezo wa kujihami.

Baada ya kuanza vizuri msimu huu, Tottenham wamerudi nyuma. Wapo nafasi ya 12 kwenye msimamo wa ligi, na wamepoteza michezo yao mitatu ya mwisho ya ligi. Harry Kane bado hajafunga bao kwenye ligi. Kwa hivyo mtu anapaswa kujiuliza wapi kichwa chake kilipo hasa baada ya sakata kali la uhamisho wakati wa majira ya joto akitaka kujiunga na Manchester City. Soka linalochezwa na Spurs kwa sasa linaonekana kuwa baya.

**#2. OLE GUNNAR SOLSKJAER (MANCHESTER UNITED)**

Ole Gunnar Solskjaer aliteuliwa kama kocha wa kudumu wa Manchester United mwaka 2019. Lakini maswali bado yanaibuka juu yake ikiwa ni kocha sahihi wa klabu hiyo.

Mtu hawezi kukataa maendeleo katika klabu tangu kuteuliwa kwa Solskjaer. Raia huyo wa Norway ameuza nyota wengi na kusajili wageni ghali. Wachezaji kama Edinson Cavani, Cristiano Ronaldo, Raphael Varane, Harry Maguire na Bruno Fernandes wote wamesajiliwa chini ya Solskjaer.

Licha ya hayo, Man United inaendelea kuwa timu isiyoendana na kiwango chake. Maono ya Solskjaer kwa Man United ni dhahiri, lakini je, Ndiye mtu sahihi kutekeleza hilo? Man United wanashika nafasi ya tatu kwenye ligi, na wamekuwa na kiwango kibaya hivi karibuni.

**#1. RONALD KOEMAN (BARCELONA)**

Barcelona wapo kwenye wakati mgumu sana. Wakati mtu anafikiria kuwa klabu kama hiyo haiwezi kushuka chini, Barcelona imeweza kufanya hivyo.

Sakata la Lionel Messi msimu huu wa majira ya joto lilikuwa la aibu vya kutosha. Lakini sasa, kuna shida kubwa zaidi kwenye klabu. Ronald Koeman ni gwiji wa Barcelona ambaye aliacha kazi ya kuinoa timu ya Taifa ya Uholanzi ili kuchukuwa jukumu la kocha wa klabu hiyo mwaka 2020. Mholanzi huyo hivi sasa yupo kwenye shinikizo kali sana.

Koeman ametoa maoni ya kutatanisha mara kwa mara katika wiki za hivi karibuni. Inasemekana alikuwa karibu kuondoka klabuni hapo msimu huu kipindi cha majira ya joto, lakini Barcelona haikuweza kupata mbadala mzuri.

Wamepoteza mechi mbili za hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich na Benfica, na wanashika nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu. Kiwango chao dimbani kimekuwa cha kushangaza. Andrea Pirlo na Xavi wamehusishwa na jukumu la kuchukua mikoba hapo Barcelona.

## ISIKUPITE

Lionel Messi ni mchezaji pekee ambaye hajacheza Ligi Kuu England anayeongoza kwa kuzifunga timu sita bora kwenye ligi hiyo; Manchester United, Manchester City, Arsenal, Chelsea, Liverpool na Tottenham Hotspur, hiyo ni baada ya kufunga mabao 27 katika mechi 35 dhidi yao, idadi hiyo ikiwa ni mabao 15 zaidi ya mchezaji yeyote yule.



NIPASHE JUMATATU OKTOBA 11, 2021





# WACHEZAJI 7 WENYE MABAO MENGI DHIDI YA 6 BORA ZA EPL



AGUERO

**LONDON,** England

LIGI Kuu England ni tajiri na bila shaka yoyote ni ligi yenye ushindani mkubwa zaidi duniani. Hiyo inaelezea kwa nini idadi kubwa ya wachezaji bora wamepamba kwenye ligi hiyo. Hao ni pamoja na Eric Cantona, Alan Shearer, Ryan Giggs, Frank Lampard, Wayne Rooney, Cristiano Ronaldo na hivi karibuni, Mohamed Salah, Ruben Dias na Kevin De Bruyne, kati ya wengine wengi.

**Wakati klabu yoyote ya Ligi Kuu England inaweza kuifunga nyingine, lakini kuna klabu sita ambazo zinasimama kichwa juu ya mabega ya wengine, kwa sababu ya ushindani na historia.**

Hizo zinajumuisha Manchester United, Manchester City, Arsenal, Chelsea, Liverpool na Tottenham Hotspur.

Isipokuwa Spurs, kila timu kati ya hizo tano zilizotajwa hapo juu zimeshinda taji la Ligi Kuu angalau mara moja. Klabu zote sita ni za kawaida kwenye mashindano ya Ulaya, na zimeshinda au kufika angalau fainali moja ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwa kuzingatia asili ya timu sita kubwa za Ligi Kuu, ni wachezaji wachache tu ambao wamefunga dhidi yao.

Kwenye makala haya, hebu tuangalie wachezaji saba wenye mabao mengi zaidi dhidi ya timu hizo kubwa sita, haya sasa...

### # 7. PIERRE-EMERICK AUBAMEYANG - 19

Pierre-Emerick Aubameyang amekuwa mfungaji mzuri katika Ligi ya England. Amefunga mabao 66, yote kwa Arsenal, katika michezo 119 kwenye misimu mitano.

Mshindi huyo wa Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora kwenye Ligi Kuu ya msimu wa 2018-19, ana mabao karibu 20 dhidi ya timu sita kubwa. Mabao yake mengi (8) amefunga dhidi ya Tottenham Hotspur.

Aubameyang amefunga dhidi ya Spurs katika mashindano matatu tofauti - Ligi Kuu (4), Ligi ya Europa (3) na Ligi ya Mabingwa Ulaya (1).

### #6. HARRY KANE - 27

Harry Kane ni mmoja wa wafungaji wenye nguvu zaidi katika historia ya Ligi Kuu. Mshambuliaji huyo wa Tottenham amefunga mabao 166 kwenye mashindano hayo, yote akiwa na Spurs.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ni mshindi mara tatu wa Kiatu cha Dhahabu, akishika nafasi za kufunga na kusaidia katika chati kwenye msimu uliopita. Kane amefunga zaidi ya mabao 20 dhidi ya timu kubwa sita za Ligi Kuu.

Mabao yake mengi dhidi ya timu hizo sita yamekuja dhidi ya Arsenal na Chelsea, ambapo amefunga mara 11 na mara sita, mfululizo. Inashangaza kwamba Kane bado hajafungua akaunti yake ya mabao msimu huu, akiambulia patupu katika kipigo cha Spurs cha mabao 3-1 kwenye Ligi Kuu kutoka kwa Arsenal.

### #5. LIONEL MESSI - 27

Lionel Messi amefunga mabao mengi dhidi ya timu kubwa sita za Ligi Kuu England. Kwa kweli, ndiye mchezaji pekee kwenye orodha hii ambaye hajawahi kucheza kwenye ligi hiyo.

Raia huyo wa Argentina, anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora zaidi waliopamba mchezo huo. Yeye ni mmoja wa wachezaji wawili kufunga zaidi ya mabao 100 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Mabao yote ya Messi dhidi ya timu hizo sita yametokea kwenye mashindano haya.

Messi, ambaye alishinda Copa America 2021 na Argentina msimu wa majira ya joto, ameifunga zaidi Arsenal. Amepachika mabao tisa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya 'Washikabunduki' hao, pamoja na manne katika mchezo mmoja. Hayo ndiyo mengi zaidi ambayo amefunga dhidi ya timu moja kwenye mashindano hayo.

Haishangazi, Messi pia amepata mafanikio dhidi ya klabu nyingine za juu kwenye Ligi Kuu. Amefunga katika fainali mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester United. Pia alifungua akaunti yake ya mabao kwa PSG kwa kufunga bao dhidi ya Manchester City, akifikisha mabao saba aliyofunga dhidi ya timu hiyo.

Messi amefunga mabao 27 katika mechi 35 dhidi ya timu za England kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya; 15 zaidi ya mchezaji mwingine yeyote kwenye mashindano hayo.

### #4. CRISTIANO RONALDO – 28

Kama Messi, Cristiano Ronaldo ni mmoja wa wachezaji bora waliowahi kucheza mchezo huu mzuri.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 alirudi kwenye ligi hiyo baada ya kuondoka miaka 12 iliyopita. Sasa ana mabao 87 kwenye mashindano, yote kwa Manchester United, katika kampeni saba tofauti za Ligi Kuu.

Mabao mengi ya Ronaldo dhidi ya timu sita za Ligi Kuu England yamekuja kwenye ligi hiyo. Klabu aliyoifunga zaidi ni Tottenham, ambapo Ronaldo ameifunga mara kumi.

Ronaldo pia amefunga mara tatu dhidi ya klabu yake ya sasa, akifanya hivyo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Bao lake pekee dhidi ya Chelsea lilipatikana katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2009, akashindwa kuwafunga katika michezo kumi ya Ligi Kuu.

### #3. EDEN HAZARD – 29

Kwa kuzingatia masaibu yake ya kufunga mabao kule Real Madrid, inaweza kushangaza kutambua kwamba, Eden Hazard amefunga zaidi ya mabao 25 dhidi ya timu sita za Ligi Kuu.

Winga huyo wa Real Madrid, wakati huo alikuwa akiichezea Chelsea, alifunga bao ambalo lilithibitisha Leicester City kama mabingwa wapya na wasiotarajiwa wa Ligi Kuu England mwaka 2016.

Hazard, mshindi mara mbili wa Ligi Kuu, alifunga mara saba dhidi ya Arsenal na Liverpool. Alifunga mara sita dhidi ya Spurs, mara tano dhidi ya Manchester United na mara nne dhidi ya Manchester City.

### #2. JAMIE VARDY – 40

Jamie Vardy Mshambuliaji wa Leicester City aliibuka kutoka kwenye fumbo na kushinda Ligi Kuu msimu wa 2015-16. Alifunga mabao 24 katika ushindi huo. Miaka minne baadaye, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alitikisa nyavu mara 23 na kushinda tuzo yake ya kwanza ya Ligi Kuu ya Kiatu cha Dhahabu.

Akiwa na mabao 123 katika misimu nane tu, Vardy ni mmoja wa wafungaji bora wa Ligi Kuu. Hajaonyesha dalili zozote za kushuka kiwango cha ufungaji, akiwa sasa ameshatikisa nyavu mara tano msimu huu.

Cha kushangaza ni kwamba mabao yake mengi ya Ligi Kuu amefunga dhidi ya timu kubwa sita. Mchezaji huyo wa zamani wa England amefunga mara 11 dhidi ya Arsenal, mara tisa dhidi ya Tottenham na mara nane dhidi ya City na Liverpool. Vardy pia amefunga mara tano dhidi ya mabingwa mara 13 wa Ligi Kuu England, Manchester United.

### #1. SERGIO AGUERO - 54

Sergio Aguero ni hadithi maarufu kwenye Ligi Kuu England. Mshindi huyo mara tano wa Ligi Kuu ndiye mchezaji pekee aliyefunga zaidi ya mabao 50 dhidi ya timu hizo sita.

Klabu tatu kati ya hizo sita, inaonekana kuwa ndio alizozionea zaidi Aguero. Mshindi huyo wa Copa America 2021, alifunga mara 15 dhidi ya Arsenal, mara 12 dhidi ya Chelsea na mara 11 dhidi ya Spurs. Pia alitikisa nyavu mara tisa dhidi ya Manchester United na mara saba dhidi ya Liverpool.

Wakati wa mafanikio ya miaka kumi katika Ligi Kuu England, Aguero (mabao 184) alikuwa mfungaji bora zaidi wa mashindano kwenye mchezo wake wa mwisho katika mashindano hayo.

Muongo mmoja baadaye, wakati Aguero anabaki kuwa sehemu ya hadithi nzuri zaidi kwenye Ligi Kuu na Man City. Alifunga angalau mara 20 katika kila msimu kwa misimu sita kati ya kumi

Hadi sasa anashikilia rekodi ya kufunga hat-trick 12 kwenye ligi hiyo.

## Nukuu


"Naipongeza timu yetu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars) kwa kutwaa ubingwa wa Mashindano ya COSAFA Wanawake 2021. Ubingwa huu unatuletea heshima, unaitangaza nchi yetu na kutia chachu kwa vijana wetu kushiriki michezo. Naipongeza TFF na wote walioshiriki kuiandaa timu yetu," **Rais wa Tanzania, Samia Suluhu.**



"Nilitaka kuondoka kwenye dirisha lililopita ili klabu ipate hela nyingi za kusajili, nimesikitishwa PSG kusema niliomba kuondoka wiki ya mwisho ya Agosti, sijapenda, wamenifanya nionekane mwizi. Niliwaambia tangu Julai sitaongeza mkataba," **Mshambuliaji wa PSG, Kylian Mbappe akijiandaa kuondoka bure msimu ujao.**



"Naipenda (Manchester United) na namna wanavyoniheshimu. Lakini sipendi kukaa benchi katika umri wangu huu, nahitaji mechi nyingi kwenye mguu wangu ili kuendelea kuwa fiti kiakili. Nahitaji kucheza na kufunga mabao mengi," **Mshambuliaji wa Man United, Edinson Cavani.**





Kiungo wa Yanga, Feisal Salum.. **PICHA: MAKTABA**

# LIGI KUU BARA KATIKA NAMBA

**Na Adam Fungamwango**

RAUNDI ya tatu Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea Jumamosi ijayo, wakati timu 16 zitakapokuwa na kazi ya kutafuta pointi tatu ili kujiweka vema kwenye msimamo wa ligi.

Ilisimama kwa muda wa wiki moja kupisha mechi zilizo kwenye Kalenda ya FIFA, hasa kusaka tiketi ya kufuzu kucheza Kombe la Dunia nchini Qatar mwakani.

Jumamosi Yanga itakuwa ugenini kwenye Uwanja wa Majimaji, Songea mkoani Ruvuma kuivaa KMC ilioamua kuipeleka mechi yake huko.

Kagera Sugar itakuwa nyumbani, Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera kuikaribisha Mbeya City, Geita Gold baada ya mechi mbili za ugenini kwa mara ya kwanza itakuwa nyumbani kucheza dhidi ya Mtibwa Sugar. Jumapili Mbeya Kwanza nayo itakuwa nyumbani, Sokoine Mbeya, kucheza dhidi ya Dodoma Jiji, huku Coastal Union ikiwa ugenini Uwanja wa Mabatini Mlandizi mkoani Pwani, kukabiliana na Ruvu Shooting.

Tayari Ligi Kuu ya Tanzania imemaliza raundi mbili huku kukiwa na matukio kadhaa yaliyojitokeza kwenye mechi hizo, ikiwamo rekodi na takwimu kadhaa ambazo katika makala haya tumezikusanya kwa mtindo wa namba, twende sasa...

**70 -** Simba ilibidi isubiri mpaka dakika hiyo kupata bao la kwanza msimu huu kwenye Ligi Kuu mchezo dhidi ya Dodoma Jiji, Uwanja wa Jamhuri, Oktoba Mosi, baada ya mechi ya kwanza kulazimishwa sare dhidi ya Biashara United, Septemba 28, mwaka huu. Bao hilo likifungwa na Meddie Kagere na kuifanya timu hiyo kuondoka uwanjani na ushindi wa 1-0.

**49 -** Ni dakika ambayo bao la kwanza la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu limefungwa. Ilikuwa ni Septemba 27 kwenye mechi ya ufunguzi Mbeya Kwanza ikicheza dhidi ya Mtibwa Sugar Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani. Alikuwa ni mchezaji William Edgar wa Mbeya Kwanza, aliyeweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga bao msimu huu. Japo siku hiyo kulikuwa na mechi tatu, lakini mechi kati ya timu hizo mbili ndiyo ilikuwa ya ufunguzi ikichezwa saa nane mchana, na Mbeya Kwanza kupata ushindi wa bao 1-0.

**23 -** Bao la kwanza la Yanga msimu huu lilifungwa kwenye dakika hiyo na Feisal Salum, Septemba 29 kwenye mechi kati ya timu hiyo dhidi ya Kegera Sugara, Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, likiwa bao pekee kwenye mchezo huo.

**22 -** Hii ni namba ya idadi ya mabao yaliyopatikana hadi kufikia raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

**18 -** Hii ni idadi ya wafungaji wa Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa ambao wote hawa kwa jumla yao wamefunga mabao 22.

**16 -** Ni idadi ya mechi zote za raundi ya pili Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea huku kila timu ikiwa imecheza mechi mbili.

**15 -** Hii ni idadi ya wachezaji wa Kibongo waliofunga mabao mpaka sasa ambao ni Vitalis Mayanga wa Polisi Tanzania, Chrispin Ngushina William Edgar wa Mbeya Kwanza, Hance Masoud wa Coastal Union, Cleophace Mkandala wa Dodoma Jiji, Peter Mapunda wa Mbeya City, Feisal Salum wa Yanga, Rashid Juma wa Ruvu Shooting, Kassim Haruna na Adam Adam wote wa Polisi Tanzania, Paul Nonga na Richardson Ngodya wa Mbeya Kwanza, Mbaraka Yusuph wa Kagera Sugar na Ralliants Lusajo wa Namungo FC.

**10 -** Ni idadi ya mechi za ushindi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka kufikia raundi ya pili.

**6 -** Inasimama kama idadi ya mechi za sare kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, zikichezwa michezo 16, kumi zikiwa zimetoa mshindi na sita zikiwa sare.

**4 -** Ni idadi ya ushindi wa mechi za ugenini ambazo zimechezwa mpaka sasa. Kwenye mechi hizo wageni wote walipata ushindi wa bao 1-0. Mechi hizo ni Yanga ilipoifunga Kagera Sugara nyumbani, Simba kuidungua Dodoma Jiji, Ruvu Shooting kuiadhibu Biashara United na Mbeya Kwanza kuiduwaza Mtibwa Sugar.

**3 -** Ni dakika ya bao la mapema zaidi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa likifungwa na Mayanga wa Polisi Tanzania, kwenye mechi dhidi ya KMC, Uwanja wa Black Rhino, Karatu jijini Arusha, Septemba 29. Kwenye mechi hiyo timu yake ilishinda mabao 2-0, akifunga yote mawili.

**2 -** Hii ni idadi ya wachezaji waliofunga mabao mawili kwenye mechi moja. Wa kwanza ni Mayanga wa Polisi Tanzania, aliyefunga mawili Septemba 29 kwenye mechi dhidi ya KMC, timu yake ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0. Mwingine ni Chrispin Ngushi wa Mbeya Kwanza, aliyefunga mawili, akisawazishia timu yake ikitoka sare ya 2-2 dhidi ya mahasimu wao wa mji mmoja, Mbeya City.

**1 -** Namba hii inasimama kwa Geita Gold kuwa ndiyo timu pekee ambayo mpaka sasa haina pointi hata moja kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, ikipoteza mechi zote mbili. Timu zote 15 kwenye ligi zimevuna angalau pointi moja.

Timu hiyo iliyoanza kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza, ilichapwa mabao 2-0 dhidi ya Namungo FC ugenini, kisha ikakutana na kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Yanga, Uwanja wa Benjamin Mkapa.

## JE, WAJUA?



KLABU ya Simba inashika nafasi ya pili kwa kuwa na wafuasi wengi (milioni 2.9) katika mtandao wa Kijamii wa Instagram ikiwa nyuma ya Al Ahly ya Misri (milioni 7.6). Raja Casablanca ya Morocco ipo nafasi ya tatu (milioni 1.9), ikifuatiwa na Zamalek ya Misri (milioni 1.7), Yanga (milioni 1.5), Wydad Casablanca ya Morocco (897K), Azam FC (875K), Kaizer Chiefs ya Sauzi (718K), Pyramids ya Misri (515K) na inayofunga 10 bora ni Orlando Pirates ya Sauzi (500K).





# Wajawazito wanavyohatarisha watoto tumboni kwa ulevi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

DAKTARI Bingwa wa magonjwa ya akili katika Hospitali ya Taifa ya Magonjwa ya Akili Mirembe, Dk. Innocent Mwombeki, ameeleza namna wanawake wanavyowaweka hatarini watoto tumboni kutokana na matumizi ya vilevi.

Dk. Mwombeki aliyasema hayo jijini hapa jana katika semina ya waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Afya ya Akili Duniani ambayo hufanyika kila mwaka Oktoba 10. Alisema matumizi ya vilevi yanasababisha watoto kuzaliwa wakiwa na matatizo ya afya ya akili.

"Mjamzito anapokunywa pombe anamweka hatarini mtoto atakayezaliwa kuwa na matatizo hayo kwa kuwa kunasababisha athari katika ukuaji wa ubongo kwa mtoto aliye tumboni na hivyo kuwa na tatizo la afya ya akili atakapozaliwa." "Tunapoangalia ongezeko la watu wenye matatizo ya afya ya akili, lazima tuangalie tangu mtoto anapokuwa tumboni, wapo kinamama wengi wanatumia vilevi wanapokuwa wajawazito, hii ina athari kwa mtoto aliye tumboni," alisema Dk. Mwombeki.

Alitaja sababu nyingine inayosababisha matatizo ya afya ya akili ni pamoja na mtoto kutolishwa vizuri tangu anapozaliwa, kufanyiwa ukatili mbalimbali, vipigo kwa watoto na manyanyaso mbalimbali.

Aliwasihi wajawazito kuacha kutumia vilevi ili kunusuru afya za viumbe vilivyo kwenye matumbo yao.

"Pia kuna wale ambao wana vinasaba vya matatizo hayo katika ukoo, akipata changamoto kidogo tu katika maisha anajikuta anapata matatizo ya afya ya akili, lakini umaskini, matatizo kazini yote hayo huchangia mtu kupata matatizo ya afya ya akili," alisema.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Shedrack Makubi, alisema takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha Watanzania milioni saba wana matatizo ya afya ya akili huku takwimu za kidunia zikionyesha watu zaidi ya milioni 300 wana matatizo hayo.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (kulia), akimsikiliza Meneja Mauzo wa Kampuni ya Kimataifa ya Usafirishaji Mizigo DHL, Abdalah Shariff, alipotembelea banda la kampuni hiyo kwenye maonyesho ya kilele cha maadhimisho ya Siku ya Posta Duniani yaliyofanyika kitaifa jijini Dodoma mwisho wa wiki. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

## Mbunge ajenga shule kuwaondolea adha wanafunzi mwendo mrefu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KUTOKANA na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Hombolo Bwawani waliopo Kijiji cha Mkoyo kutembea umbali wa kilometa tisa kila siku kufuata masomo, Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde kwa kushirikiana na wananchi ameanzisha ujenzi wa shule mpya ili kuondokana na tatizo hilo.

Akizungumza mwishoni mwa wiki aliposhiriki uchimbaji msingi wa madarasa, Mavunde alisema wameamua kujenga shule mpya ya sekondari ya Mkoyo ili watoto hao waondokane na adha hiyo na ni sehemu ya mkakati wake wa kuboresha sekta ya elimu jimboni humo.

"Mwanafunzi kutembea umbali mrefu kuna athari nyingi wengine hulazimika kukatisha masomo yao, hivyo tumeona ili kuondokana na hilo tusogeze shule kwenye eneo lao," alisema.

Aliwashukuru wananchi kwa kujitolea nguvukazi kwa ajili ya ujenzi huo ambao utawapunguzia mwendo wanafunzi wa Mkoyo.

"Katika kuanzisha mchakato wa ujenzi huu wa ujenzi wa madarasa kwa ajili ya sekondari, nimechangia kokoto, saruji mifuko 100 na matofali 2000," alisema.

Awali, katika ujenzi wa Shule ya Msingi Ngh'ole, alichangia matofali 1,000 na saruji mifuko 80 huku shule mpya ya Ndachi akichangia matofali 2,000 na saruji mifuko 130.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi, Diwani wa Hombolo Bwawani, Assed Ndajilo, alimshukuru Mavunde kwa kuwa chachu ya maendeleo katika kata hiyo na kuahidi kuendelea kumpa ushirikiano ili kukamilisha miradi yote aliyoianzisha.

# Tanzania yaweka miradi kimkakati Expo 2020 Dubai

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TANZANIA imechagua miradi kadhaa ya kimkakati kwa ajili ya kuitangaza duniani kupitia maonyesho ya dunia ya Expo 2020 yanayofanyika jijini Dubai.

Miradi hiyo ni mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), reli ya kisasa (SGR) upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, ujenzi wa viwanja vya ndege na kuimarisha usafiri wa anga.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa kuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maonesho hayo ambayo yameanza Oktoba mosi, mwaka huu hadi Machi 31, mwakani.

Alisema maonyesho hayo mwaka huu yanalenga kuunganisha mawazo kwa ajili ya mstakabali wa kesho na kutatua vikwazo vinavyoikabili dunia kwenye sekta ya biashara, kilimo, mazingira, mabadiliko ya tabia nchi, nishati, madini, utalii, viwanda na teknolojia.

"Kwa kuzingatia hili Tanzania kwenye maonyesho haya imechagua baadhi ya miradi kwenda kuonesha duniani kuonyesha kitu gani tunafanya katika kutatua changamoto mbalimbali, kwenye nishati tunaenda kuonesha mradi wetu wa kufua umeme, miundombinu tumechagua SGR, upanuzi wa Bandari Dar es Salaam, ujenzi na upanuzi wa viwanja mbalimbali vya ndege," alisema.

Alisema Tanzania imejipanga vyema kutatua tatizo la miundombinu na nishati katika ujenzi wa viwanda.

"Kwenye usafiri wa anga katika kuwaleta watalii hapa nchini tunatangaza watasafiri ndani ya nchi na kutembelea maeneo mbalimbali bila usumbufu mkubwa," alisema.

Kadhalika, alisema serikali inashirikiana na sekta binafsi kuonyesha bidhaa zinazozalishwa nchini ikiwamo za kilimo, ngozi na mazao mbalimbali.

"Hadi sasa tayari taasisi mbalimbali 27 zinaonyesha bidhaa mbalimbali kule Dubai ikiwamo watu wetu wa utalii kuhakikisha maeneo yetu ya vivutio yanatangazwa kikamilifu na dunia kuviona na tunatarajia baada ya maonyesho tutapata watu wengi kuja kututembelea," alisema.

Alisema Kituo cha Uwekezaji (TIC) kipo pia kwenye maonyesho hayo kwa lengo la kutangaza fursa za uwekezaji ili kupata wawekezaji na wafanyabiashara kuwekeza Tanzania.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara na sekta binafsi kuchangamkia fursa ya ili kujitangaza zaidi kimataifa kupitia bidhaa mbalimbali walizo nazo na kupata masoko ya uhakika.

Awali, alibainisha kuwa maonyesho hayo hufanyika kila baada ya miaka mitano, awali yalipangwa kufanyika kuanzia Oktoba mosi 2020 hadi Machi 31, 2021, lakini uwapo wa ugonjwa wa Uviko-19 yalisogezwa hadi Oktoba mwaka 2021.

Waziri huyo alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi 191 ambazo zinashiriki maonyesho hayo na uratibu wake unafanywa na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (Tantrade).

# Aomba uharaka ujenzi barabara Ikukwa-Kawetere

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, ameiomba serikali iharakishe ujenzi wa Barabara ya Ikukwa-Kawetere yenye urefu wa kilomita 40 ili kuwapunguzia wananchi wa Kata ya Ikukwa umbali wa kusafiri kwenda kupata huduma muhimu jijini Mbeya.

Alitoa ombi hilo wakati wa ziara yake ya kusikiliza kero za wananchi wa kata hiyo akiongozana na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua pamoja na wataalamu mbalimbali wa halmashauri wakiwamo maofisa kutoka Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

Alisema barabara hiyo ni muhimu kiuchumi kwa wananchi wa Kata ya Ikukwa na kata za jirani za Wilaya ya Chunya ikiwamo Kata ya Ifumbo kutokana na kuwa ya mkato kwenye usafirishaji wa mazao mbalimbali yanayozalishwa katika ukanda huo.

Alisema wananchi wa kata hizo wanalima mahindi, ufuta, karanga maharagwe na uchimbaji wa madini ya dhahabu hasa katika Kata ya Ifumbo na kwamba barabara hiyo ni muhimu kwa usafirishaji wa vitu hivyo.

Alisema kwa sasa wananchi hao wanalazimika kusafiri umbali wa zaidi ya kilomita 70 kwa kupita barabara ya Ikukwa-Njelenje-Mbalizi ambayo hata hivyo alisema siyo nzuri kutokana na maeneo mengi kuwa na mashimo.

"Hii barabara itakuwa imewapunguzia wananchi hawa zaidi ya kilomita 30, hawa ni wazalishaji wazuri sana wa mazao mbalimbali ya chakula na biashara, lakini masoko ya kuuzia mazao haya yapo Mbeya Mjini, hivyo hii barabara ni muhimu sana na ni ya mkato sana," alisema Njeza.

Vilevile, aliiomba serikali kuweka mkazo kwenye uboreshaji wa barabara ya Ikukwa-Njelenje-Mbalizi ambao alisema ina umuhimu wake kwa wananchi wa kata hiyo. Mwakilishi wa Meneja wa TARURA wa Wilaya ya Mbeya, Arcard Tesha, alisema wanaendelea na ujenzi wa barabara hiyo kwa awamu tofauti kulingana na upatikanaji wa fedha.

Alikiri kuwa barabara hiyo ni muhimu kwa wananchi wa kata hiyo huku baadhi ya madaraja muhimu yamekamilika na mkandarasi anaendelea kuchonga barabara hiyo ili kuunganisha maeneo muhimu yaliyobakia.

"Mwaka juzi mkandarasi alijenga kilomita sita na sasa anaendelea na eneo hilo ambalo tumetoka kuliangalia na mradi huu kwa sasa una bajeti ya Sh. milioni 276 na mitambo ipo kazi inaendelea," alisema Te Alisema pia wameomba Sh. bilioni 1.3 kwa ajili ya kuboresha barabara ya Ikukwa - Njelenje ambayo ndiyo inayotumika kwa sasa na wananchi wa maeneo hayo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Chuachua, aliagiza watendaji wa TARURA kuhakikisha barabara hiyo ya Ikukwa-Kawetere kupitia Mlima Mbeya inakamilika mapema ili wananchi hao waanze kunufaika kwa kusafirisha mazao yao.



Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza (kushoto), akimwonyesha Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua (kulia), mahali itakakopita barabara ya Ikukwa-Kawetere yenye urefu wa kilomita 40, viongozi hao walifanya ziara katika eneo hilo hivi karibuni kwa lengo la kuhamasisha kasi ya ujenzi wa barabara hiyo kuongezeka. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# EWURA yazionya Mamlaka za Maji ukataji maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imezipiga marufuku Mamlaka za Maji nchini kuwakatia wananchi huduma za maji siku za mwisho wa wiki na sikukuu ili kuwashinikiza kulipia huduma hiyo.

Ofisa Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mafunzo maalumu kuhusu masuala ya udhibiti kwa waandishi wa habari 70 kutoka katika mikoa sita ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yaliyoandaliwa na mamlaka hiyo na kufanyika jijini Mbeya.

Mikoa ambayo ilikuwa na wawakilishi kwenye mafunzo hayo ni Ruvuma, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi na waandishi hao walikuwa wanafundishwa ili wabobee kwenye habari za udhibiti.

Kaguo alisema mwananchi ambaye hajalipia huduma ya maji anatakiwa kusitishiwa huduma siku za kazi ili kumpa nafasi kwenda kulipia na kurejeshewa huduma kwa wakati na kuonya siku za mwisho wa wiki na siku za sikukuu hata mamlaka hizo zinafunga ofisi.

Alisema EWURA iliamua kupiga marufuku hiyo kutokana na baadhi ya watendaji wa mamlaka hizo kutumia mwanya huo kuwakomoa wananchi na kuwanyima haki yao na kwamba wameweka utaratibu kwamba mwisho wa kusitisha huduma kwa wananchi ni Alhamisi.

"Mamlaka ikikiuka katazo hili tukapata malalamiko tunachukua hatua kali dhidi ya mkurugenzi, kwanza tutamwonya na akiendelea tuna nafasi ya kumshauri Waziri wa Maji kuchukua hatua zaidi ikiwamo kumuondoa kwenye nafasi hiyo," alisema Kaguo.

Alisema ili kukabiliana na tatizo hilo pia wameanza kuzishauri Mamlaka za Maji nchini kuwafungulia wananchi dira za Lipa Kabla (LUKU) kama ilivyo kwa Shirika la Umeme nchini (TANESCO).

Vilevile, alisema ili kukabiliana na tatizo la wananchi kulalamika kubambikiwa ankara kubwa za maji, wamepiga marufuku wasoma dira wa mamlaka za maji kusoma nyumbani kwa mtu bila mhusika kuwapo.

Alisema wasoma dira wanatakiwa kusoma dira kwa kushirikiana na mwenye nyumba ama mtoto, baada ya hapo anatakiwa akifika ofisini wakati anapoandaa ankara anatakiwa kumtumia ujumbe wa simu mhusika kumjulisha kiwango cha maji yaliyotumika ili na yeye ajiridhishe kama kilichoandikwa ni sawa na kilichosomwa.

Baadhi ya waandishi wa habari walishauri serikali kupitia EWURA kudhibiti mfumuko wa bei ya mafuta kwa kuweka bei moja nchi nzima kama ilivyo kwenye mataifa mengine ikiwamo Zambia ambako walidai nchi nzima ni bei moja.

Mmoja wa waandishi hao, Hosea Cheyo kutoka Katavi alisema kumekuwa na tatizo la mafuta kuwa bei juu nchini huku baadhi ya mataifa ambayo yanapitisha mafuta Tanzania kuuza bidhaa hiyo kwa bei ya chini.

Alisema kwa sasa nchini Zambia bei ya mafuta ni moja katika nchi nzima na iko chini kuliko ilivyo Tanzania hali hiyo inawafanya baadhi ya Watanzania wanaoishi kwenye maeneo ya mipakani ikiwamo Tunduma kuvuka mipaka na kwenda kusaka bidhaa hiyo upande wa pili.

"Zambia wanasafirisha mafuta kutoka bandari yetu ya Dar es Salaam yakifika kwao yanawekwa vinasaba na kusambazwa nchi nzima ambako yanauzwa kwa bei moja maeneo yote, sasa kwetu inashindikana nini?" Alihoji Cheyo.

## Wakulima walia na bei ya mbolea, pembejeo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA mkoani Mbeya wameiomba serikali kutafuta namna ya kupunguza bei ya mbolea pamoja na pembejeo zingine ili kuwasaidia kuongeza uzalishaji na kupata tija zaidi.

Wananchi hao walitoa ombi hilo juzi wakati wa uzinduzi wa duka la pembejeo la kampuni ya ukopeshaji wa pembejeo ya One Acre Fund lililopo katika Kijiji cha Imezu Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na kusema kwa sasa bei ya mbolea ipo juu kuliko miaka yote.

Mmoja wa wananchi hao, Joseph Mbuna alisema kwa sasa bei ya mbolea haiendani na ya mazao hali ambayo itasababisha wananchi kushindwa kumudu bei hizo na kushuka kwa uzalishaji wa mazao.

Alisema kwa sasa bei ya mbolea ni kuanzia Sh. 80,000 na kuendelea wakati ya mahindi ambayo yalivunwa msimu uliopita yanauzwa kwa bei ya kati ya Sh. 3,500 na 6,000 katika Mkoa wa Mbeya na kwamba ili mwananchi anunue mfuko wa mbolea atahitaji kuuza mahindi mengi.

"Mwaka huu bei ya mbolea imekuwa tatizo kubwa sana, itatufanya wakulima tusizalishe kabisa, tunaomba serikali itusaidie kukabiliana na tatizo hili," alisema Mbuna.

Mwakilishi wa One Acre Fund wa mikoa ya Mbeya na Songwe, Erica Kafwimi, alisema waliamua kufungua duka hilo ili kuwarahisishia wakulima kupata mbolea na pembejeo zingine kwa wakati na kuondoa tatizo la wananchi kuuziwa pembejeo feki.

Alisema wamekuwa wakifanya kazi na wakulima kwa muda mrefu hasa kwenye ukopeshaji wa pembejeo za kilimo na kwamba kwa sasa wataendelea kuwahudumia wananchi wa maeneo yote ambayo wamekuwa wakiyahudumia.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka wafanyabiashara kuendelea kupunguza bei za mbolea ili wananchi wengi waendelee kutumia na kuongeza uzalishaji.

Alisema serikali inaendelea na juhudi mbalimbali za kukabiliana na tatizo hilo la mfumuko wa bei ya mbolea ili wananchi waendelee kuzalisha kwa tija.



# Dozi 70,000 chanjo corona Z'bar haijatumika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazuri, amesema bado mwamko wa wananchi wa Zanzibar kuchanja chanjo ya corona ni mdogo na kuna mrundikano mkubwa wa dozi ya chanjo hizo.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na Nipashe kuhusu mwamko wa wananchi kuchanja chanjo ya corona.

Waziri Mazrui, alisema Serikali ya Zanzibar ilipokea dozi ya corona 100,000 lakini zilizotumika ni dozi 30,000 na bado dozi 70,000 hazijatumika.

"Tumepokea dozi ya chanjo ya corona laki moja lakini zilizotumika hadi sasa ni thelathini elfu tu....tuna dozi ya Sputnik ya nchini Urusi elfu thelathini, Jonsonjonson ya Marekani thelathini na tano elfu, Sinovac ya Kichina tunazo hamsini na tano dozi zilizotumika hatujafikia hata nusu yake, lakini tunataka tujitahidi angalau ifikapo Desemba mwaka huu kufikia nusu ya dozi zilizotumika," alisema Waziri Mazrui.

Alisema chanjo za Sinovac kutoka China muda wake wa kuharibika ni miaka miwili na kwamba kama wananchi hawatochanja hazitofaa tena ikifika miaka miwili.

Alisema serikali imesogeza chanjo ya corona katika vituo mbalimbali mjini na vijini ili kuwarahisishia wananchi kuchanja, lakini bado mwamko ni mdogo kutokana na baadhi ya wananchi kuwa na dhana potofu dhidi ya chanjo hizo.

"Bado baadhi ya wananchi wanaamini kuwa wakichanja chanjo ya corona watakuwa mazombi jambo ambalo sio kweli mimi nimeshachanja chanjo ya Sinovac na Jonsonjoson na sijawa zombie nawaomba wananchi wasiogope wakachanje," alisema Mazrui.

Alisema wananchi waliochanja kwa wengi ni chanjo ya Sinovac ya China ambayo ilianza mwanzo kutolewa, lakini kwa sasa wanaochanja kwa wingi ni ya Jonsonjonson.

Alisema kama watu hawatochanja ikiwamo wafanyakazi wa hoteli na wataalamu wa afya nchi itakosa watalii na kushindwa kupata fedha zitokanazo na sekta hiyo ambayo ndio sekta mama serikali inayotegemea kupata fedha.

"Kwa kweli bado mwamko ni mdogo sana wa wananchi kuchanja cha kusikitisha zaidi hata hao baadhi ya wataalamu wa afya hawataki kuchanja," alisema. Aliwataka wananchi kuchanja ili kusaidia taifa na uchumi wa nchi pia kusaidi kutoeneza maambukizi ya corona kwa watu wengine.

Alisema Wachina wameshachanja zaidi ya bilioni 1.1 nchini kwao, na wataalamu wa afya wameshafanya uchunguzi chanjo ya corona hazina madhara yoyote na kuwataka wananchi kujitokeza kuchanja.

Alisema katika watu waliojitokeza kuchanja chanjo ya corona kwa Zanzibar Mkoa wa Mjini Magharib Unguja unaongoza, aliwataka wakuu wa mikoa kuwahamasisha wananchi wao kuchanja.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi wa Hoteli ya Melia iliyopo Kiwengwa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Nicolas Konig, amewaongoza wafanyakazi wa hoteli hiyo kupata chanjo ya corona ili kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha wananchi kupatiwa chanjo ili wananchi kuishi salama na ameamua kuongozana na wafanyakazi wake kupata chanjo hiyo.

Alisema ameamua kuwaita wataalamu wa afya hotelini hapo ili kuwarahisishia wafanyakazi wake kupata chanjo hiyo hasa ikizingatiwa kuwa wanawahudumia wageni kutoka mataifa mbalimbali wanaofika hotelini hapo.

Mkurugenzi huyo alifahamisha kuwa wawekezaji wengi wanajivunia ushirikiano uliyopo baina ya serikali hasa katika mambo muhimu ikiwamo ya afya.



Wanafunzi wa Shule ya Mkwajuni Mkoa wa Kaskazini Unguja wakitoa igizo la ngonjera katika viwanja vya Shule ya Mkwajuni wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani ambayo huadhimishwa Oktoba 11 ya kila mwaka. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Watoto wa kike wahitaji walimu wa sayansi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kusherehekea Siku ya Mtoto wa Kike Duniani, watoto wa kike wamesema kuwa wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo uhaba wa walimu wa sayansi hali ambayo inasababisha kutofanya vizuri katika mitihani yao ya taifa.

Wakizungumza katika hafla ya shamrashara za kusherehekea siku hiyo iliyofanyika katika Kijiji cha kulelea watoto Zanzibar (SOS), walisema kutokana na uhaba wa walimu wa sayansi pamoja na ukosefu wa maabara kwa baadhi ya shule kunasababisha watoto hasa wa kike kukimbilia katika masomo ya sanaa.

Fatma Juma Gora, mwanafunzi wa Shule ya Jongowe Kaskazini Unguja, alisema shuleni kwao kuna uhaba wa vifaa vya sayansi, walimu wa masomo ya Sayansi na Hesabati na kupata matokeo mabaya katika masomo hayo.

Aliiomba serikali kupita katika shule zao kuangalia chagamoto zinazowakabili hasa wanafunzi wa kike ambao wanapitia katika mazingira magumu kupata elimu.

Akizungumza katika sherehe hizo, Ofisa Miradi kutoka Kijiji cha Kulelea Watoto, Nyezuma Simai, aliitaka jamii kuiona thamani ya mtoto wa kike katika kuwaendeleza kielimu na kwa kuwapa fursa sawa na mwanadamu yoyote bila ya ubaguzi.

Alisema mara nyingi watoto wa kike kila wanapofikia umri wa kubalehe au elimu ya juu, huoenakana kama elimu sio haki yao tena na fursa hizo hiyo hupewa zaidi kwa watoto wa kiume.

Kadhalika, alisema hivi sasa Tanzania inaongozwa na Rais mwanamke ambaye kama angekuwa hakukuzwa na familia yake asingekuwa na nafasi hiyo, lakini kipaji chake hakikudharauliwa na kusisitiza wasidharauliwe badala yake wawepe nafasi.

"Siku ya mtoto wa kike, imekuja katika kupambania haki yenu lakini unapambaniwa na wewe uwe tayari na namna bora ya kupambania haki yako hasa katika masomo," alisema.

Naye Mratibu wa mradi wa kuimarisha familia wa Kijiji cha SOS, Mwanaidi Ali Said, alisema kijiji chao wanaendeleza watoto kwa kuwafanya wawe wakakamavu na kujitambua ili wawe na mafanikio.

Hata hivyo, alisema kupitia mradi huo wamekuwa wakiwahamasisha watoto wa kike kupata maendeleo na kujitambua ili kuwa na mwelekeo mzuri wa maisha yao.

## Rasimu sera kinga usafirishaji haramu binadamu yaiva

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Christopher Kadio, amesema rasimu ya sera ya kinga ya usafirishaji haramu wa binadamu na kinga ya uhamiaji haramu katika Bara la Afrika, inatarajiwa kufikishwa kwa mawaziri husika ili kuthibitishwa rasmi kwa lengo la kupiga vita biashara haramu Afrika.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya sera hizo kujadiliwa kwa kina na timu ya kiufundi kutoka mataifa 55 ya Umoja wa Afrika (AU), katika kikao maalumu kilichoandaliwa na Tume ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Afrika(AUC), kilichofanyika kwa muda wa siku tatu mjini hapa.

Kadio alisema majadiliano ya sera hizo yamefikiwa katika hatua nzuri ambayo yatasaidia kuongeza nguvu ya kupambana na uhalifu huo unaosababisha uvunjifu wa haki za binadamu kwa Waafrika.

Alisema, Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazopiga vita usafirishaji haramu wa binadamu na kufanyika kwa majadiliano hayo kutaziwezesha nchi za Afrika ikiwamo Tanzania kuwalinda raia wake na kuwaweka salama.

Alisema Serikali ya Tanzani inapinga kwa kiasi kikubwa biashara hiyo kwa vile inajua madhara yake na wanaopata tabu zaidi ni wanawake na watoto kudhalilishwa na kuondolewa utu wao.

Kadhalika, alisema watahakikisha kuwa wakati wote Tanzania inakuwa salama juu ya uharamia huo kwa vile serikali hiyo imesaini mikataba mbalimbali ya kimataifa na haki za binadamu na imeshawahi kuwahifadhi wakimbizi kutoka nchi mbalimbali za Afrika.

Alisema mkutano huo ulikuwa na ajenda ya kujadili sera ya kupinga vitendo hivyo na hapo baadaye kukutana mawaziri husika wa bara la Afrika na kupitisha lazima biashara hiyo haitakuwa na nafasi kubwa kwa kuwa mazimio yatafanya kazi zake kwa nchi husika na kuyafuata.

Naye Katibu Sekretarieti ya Kitaifa ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu, Seperatu Fela, alisema mkutano huo umewawezesha wajumbe kuzipitia sera na utasaidia kuwaunganisha Waafrika ili kupata nguvu ya pamoja ya kupiga vita uhalifu huo.

Alisema, jitihada zinazoendelea kufanywa na wanajumuiya wa Umoja wa Afrika zitasaidia kwa kiasi kikubwa kupiga vita usafirishaji wa binadamu kwa njia ya haramu pamoja na uhamiaji haramu.

Miongoni mwa sababu zinazosababisha Waafrika kufanyiwa uhalifu huo ni umaskini, ukosefu wa ajira pamoja na machafuko ya kisiasa.

Miongoni mwa mapendekezo yaliyotolewa katika mkutano huo ni kufanyika kwa mazungumzo baina ya wanaharakati wa Afrika wanaopiga vita uhalifu huo na mataifa yanayoshiriki katika uhalifu huo nje ya Afrika.

# Saba wanusurika kifo cha moto

**Na Richard Makore,** MWANZA

WATU saba wa familia moja katika mtaa wa Magomeni eneo la Kirumba, wilayani Ilemela mkoani Mwanza, wamesurika kifo baada nyumba yao kushika moto na kuteketea jana majira asubuhi.

Moto huo ambao chanzo chake hakijajulikana, ulianza kuwaka majira ya saa 1.40 asubuhi na kusababisha baadhi ya vitu vya ndani kuteketea huku watu waliokuwamo ndani wakijiokoa na kutoka nje.

Akizungumza katika eneo la tukio, askari wa zamu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji jijini Mwanza, Sajenti Daudi Mlelwa, alisema baada ya kupata ajali hiyo walikimbia haraka na kufika eneo la tukio.

Alisema baada ya kufika walisubiri mafundi wa Shirika la Umeme Nchini (TANESCO) wafike kwa ajili ya kukata umeme ili Zimamoto waanze kazi ya kuzima moto huo.

Alisema ingawa TANESCO walichelewa kidogo, lakini walifika na kukata umeme na baada ya hapo Zimamoto walianza kazi yao na kufanikiwa kuokoa vyumba saba kati ya 10 katika nyumba hiyo.

Vyumba vitatu viliteketea, lakini walifanikiwa kuokoa vyumba saba huku watu wote saba waliokuwa ndani ya nyumba hiyo walijiokoa.

Kutokana na moto huo, aliwakumbusha wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ili kupambana na majanga ya namna hiyo.

Kwa upande wake, mmiliki wa nyumba hiyo, Emanuel Ng'hambi, alisema mapema jana asubuhi walisikia sauti za watoto wakipiga kelele za kuomba msaada kwamba kuna moto unawaka.

Alisema baada ya kusikia kelele hizo aliingia ndani na kukuta moto ukiendelea kuwaka na kuamua kupiga simu kwa Jeshi la Zimamoto kuomba msaada.

Alipongeza jeshi hilo kwa kufika kwa wakati eneo la tukio wakiwa na vifaa vyote na kufanikiwa kuzima moto na kuokoa vyumba saba kati ya 10.

Akizungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa Serikali za Mtaa, Abdalah Seleman alisema, moto huo ulinza kidogo kidogo ukianzia chumba cha watoto.

Alisema nyumba hiyo hivi karibuni ilifanyiwa ukarabati na kwamba haijulikani chanzo cha moto huo.

Alilipongeza Jeshi la Zimamoto pamoja majirani walioonyesha upendo kwa kushiriki kuzima moto huo na hivyo kuepusha madhara makubwa ambayo yangetokea ikiwamo kuteketea vyumba vyote.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akimkabidhi Meneja Mwandamizi wa TBL Plc, Amanda Walter, kwa niaba ya kampuni tuzo ya Rais ya Mzalishaji Bora baada ya kuibuka mshindi wa pili wakati wa hafla ya kutoa tuzo iliyofanyika Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, wapili kutoka kulia ni Waziri wa Viwanda, Kitila Mkumbo na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala. Kulia ni Meneja Mauzo ya Nje wa TBL, Maleke Mringo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Ashikiliwa madai kuua mama

**Na Elizabeth Zaya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linamshikilia Julius Mzava (26) mkazi wa Chang`ombe wilayani Temeke kwa tuhuma za kumuua mama yake mzazi, Magdalena Peter (56).

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Kanda hiyo, Muliro Jumanne, mtuhumiwa huyo alimuua mama yake huyo kwa kumchoma na kisu sehemu ya mwili wake.

"Tukio hili limetokea Oktoba 10, mwaka huu, saa moja na nusu usiku eneo la Sandali, Chang`ombe baada ya kuingia chumbani kwa mwanawe Julius kwa nia ya kumpelekea chakula, ndipo aliposhambuliwa kwa kisu eneo la mwili wake akapata majeraha makubwa yaliyosababisha apoteze maisha, licha ya jitihada za kumpeleka hospitali kufanyika," alisema Muliro.

Alisema tayari mtuhumiwa huyo amekamatwa na anahojiwa kwa kina na atafikishwa mahakamani kwa hatua muhimu za kisheria. Katika tukio jingine, Muliro alisema, Jeshi la Polisi Kanda hiyo ya Dar es Salaam limewakamata na linawashikilia watu watano kwa tuhuma za kujihusisha na wizi vya vifaa vya magari na kupokea vipuri vya magari vya wizi.

"Watuhumiwa hao walikamatwa na vifaa mbalimbali vya magari zikiwamo taa za magari aina ya Toyota IST na milango ya magari ya aina mbalimbali," alisema.

"Pia, vitu mbalimbali vilivyokuwa vimeibiwa na wahalifu kwenye matukio tofauti ya uvunjaji vimekamatwa katika Kituo cha Polisi Goba yakiwamo majenereta zaidi ya 25, vifaa mbalimbali vya ujenzi na mitungi ya gesi 10."

# Serikali: Tunatambua mchango wa NGO

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema inatambua mchango wa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), na kwamba kazi wanazofanya ni muhimu na zinaisaidia katika kufikia malengo yake ya kimaendeleo na pia kuboresha maisha ya wananchi.

"Mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na wadau wengine wa maendeleo wanasaidia serikali katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Sekta hii inakuwa kwa kasi ikiwa ni pamoja na kutoa mchango katika kuwajengea uwezo Tanzania hasa wanawake na vijana," alisema Msajili wa NGO, Vickness Mayao, alipokuwa akizungumza katika hafla ya maadhimisho ya miaka 50 ya Shirika la SNV Tanzania, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Mayao alisema malengo ya SNV Tanzania yanaendana na malengo ya serikali kwenye sekta wanazifanyia kazi ikiwamo mabadiliko ya tabia nchi, usawa wa kjinsia, kilimo na uwezeshaji wanawake na vijana.

Alisema shirika limeweza kuwajengea uwezo wanawake iliwaweze kushiriki katika katika kutoa maamuzi katika ngazi ya familia na makazini.

Msajili alisema kuwa SNV kupitia mradi wake wa fursa na ajira kwa vijana (Opportunities for Youth Employment-OYE) imewezesha upatikanaji wa ajira kwa vijana wengi ambapo kati yao asilimia 2 ni wanawake.

Tangu mwaka 2013, Shirika la SNV Tanzania limetoa mafunzo ya stadi za maisha kwa vijana 18,000 ambapo asilimia 42 kati yao ni wanawake.

Mayao alisema shirika linafanya kazi katika sekta muhimu ikiwamo ya huduma ya maji, usafi na kujisafi (WASH), kilimo (mabadiliko ya tabia nchi) na nishati jadidifu. Alisema kupitia mradi wa WASH wato wamehamasika na wanazingatia taratibu za kujisafi.

Naye Balozi wa Uholanzi nchini, Weibe de Boer, alisema maelfu ya wanaojitolea kupitia shirika hilo wanalenga kuleta mabadiliko katika jamii. Alisema SNV ilianzishwa nchini mwaka 1965 kama muunganiko wa watu wanaojitolea, lakini imekuwa ikikua kadiri miaka inavyosogea, hata kuacha kufanya kazi moja kwa moja na serikali na kuwa shirika huru linalojitegemea mwaka 2002.

"Tulichagua Tanzania kwa mradi wa WASH na ule wa mabadiliko ya nchi ambao uko zaidi katika kilimo; tunasaidia wakulima wadogo kuweza kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Mpaka sas tumeweza kuwasaidiza wakulima wadogo 100,000," alisema Balozi de Boer na kuongeza kuwa wametoa vifaa vya umeme wa jua kwa watu 100,000 wanaoishi maeneo ya vijijini.

Mkurugenzi Mkazi wa SNV, Duncan Rhind, alisema: "Kwenye mradi wetu wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi tunawapa zaidi kipaumbele wanawake. Tunalenga kuleta mabadiliko chanya katika maisha ya watu na pia kuwawezesha kupata huduma muhimu."

Alisema baadaye SNV ilifanikiwa kujikuta imewezesha Watanzania wengi kupata ujuzi kupitia programu yake ya kuwaleta wataalamu wa kujitolea wenye ujuzi na uzoefu mkubwa, alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa SNV Global, Megan Ritchie, alisema kuwa wakiwa wamefanya kazi Tanzania kwa miaka 50, bado wamejizatiti kuendelea kutekeleza miradi mbalimbali kwa kufanya kazi na makundi tofauti ikiwamo serikali, wadau wa maendeleo, sekta binafsi, asasi zisizo za kiserikali na jamii. Alisema SNV inafanya kazi katika nchi nyingi zikiwamo za Afrika, Asia na Amerika ya Kati.

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## MASWALI NA MAJIBU KUHUSU UTARATIBU WA UHAMISHAJI UMILIKI WA VYOMBO VYA MOTO

**1. Swali: Chombo cha moto ni nini?**
**Jibu:** Ni chombo kinachotumika katika usafirishaji ardhini, ambavyo ni pamoja na magari, pikipiki na bajaji.

**2. Swali: Nikitaka kununua gari kwa mtu taratibu zikoje?**
**Jibu:** Unapaswa ufike ofisi ya TRA na picha ya pasipoti ya muuzaji, ripoti ya ukaguzi kutoka kwa trafki, barua ya muuzaji kuhusu mabadiliko ya umiliki wa gari, picha yako ya pasipoti, kadi halisi ya gari, hati ya kiapo ya muuzaji, gari kufika TRA kwa ajili ya ukaguzi, mkataba wa mauziano uliothibitishwa na mwanasheria na upewe risiti ya EFD kutokana na huduma ya kisheria.

**3. Swali: kumwakilisha mtu kwenye taarifa za uhamishaji wa chombo inaruhusiwa?**
**Jibu:** Ndiyo, kwa kampuni au taasisi unaruhusiwa kwa mwakilishi kuleta idhini maalum ya kisheria *(Power of Artoney)* ya kuthibitisha uwakilishi wake lakini kwa mtu binafsi anapaswa awepo mhusika mwenyewe.

**4. Swali: Taarifa za mabadiliko ya umiliki wa chombo cha moto zinatakiwa ziwasilishwe lini? Jibu:** Taarifa ya maabadiliko ya umiliki wa chombo cha moto yanatakiwa yafanyike ndani ya siku 7 baada ya kuandikishiana mkataba wa mauziano.

**5. Swali: Gharama za uhamisho wa umiliki wa chombo cha moto hulipwa lini?**
**Jibu:** Gharama za uhamisho wa chombo cha moto zinapaswa kulipwa ndani ya siku 30 baada ya mauziano kufanyika.

**6. Swali: Gharama ya kuhamisha umiliki wa gari ni shilingi ngapi?**
**Jibu:** Ada ni **shilingi 50,000/=** jumlisha ada ya nakala ya kadi ambayo ni **shilingi 50,000/=**, jumlisha na ushuru wa stempu ambao ni **asilimia 1** ya bei ya gari.

**7. Swali: Gharama ya kuhamisha umiliki wa bajaji, Je?**
**Jibu:** Ada ni **shilingi 27,000/=** jumlisha ada ya nakala ya kadi ya **shilingi 30,000/=** jumlisha ushuru wa stempu ambao ni **asilimia 1** ya bei ya bajaji.

**8. Swali: Gharama ya kuhamisha umiliki wa pikipiki nao upoje?**
**Jibu:** Ada ya uhamisho ni **shilingi 27,000/=** jumlisha ada ya nakala ya kadi ambayo ni **shilingi 20,000/=** jumlisha ushuru wa stempu ambao ni **asilimia 1** ya bei ya pikipiki.

**9. Swali: Kuna ulazima wa kubadilisha taarifa za umiliki TRA?**
**Jibu:** Ndiyo, unapaswa kubadili taarifa za chombo TRA ili umiliki uhame kutoka kwako kwenda kwa mtu mwingine la sivyo kuna athari zinaweza kutokea.

**10. Swali: Athari za kutobadili umiliki au taarifa ya chombo cha moto ni zipi?**
**Jibu:** Athari zinazoweza kutokea ni
- **(i)** Mmiliki wa awali anaweza kuwajibishwa endapo chombo kitatumika kwenye uhalifu,
- **(ii)** Mmiliki mpya atakosa malipo ya fidia kutoka bima,
- **(iii)** Mmiliki mpya atakosa uhalali wa kutumia chombo hicho kama dhamana ya kukopa,
- **(iv)** Mmiliki wa awali atawajibika endapo mmiliki mpya atakopa kwa kutumia chombo hicho.

# MBUNGE WA RORYA AJITOSA KUNOGESHA UMOJA CUP 2021

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI michuano ya Umoja Cup Rorya 2021, ikiendelea wilayani humo mkoani Mara, Mbunge wa wilaya hiyo, Jafari Wambura Chege, amenogesha utamu kwa kuongeza chachu baada ya kutoa neno lililowakuna mashabiki, timu shiriki na wadau wa soka kwa ujumla.

**Mashindano hayo ambayo kwa sasa yapo hatua ya makundi kwa timu 20 kugawanywa katika makundi manne, yanadhaminiwa na mdau wa soka wilayani Rorya, Peter Owino kwa mwaka wa tisa sasa.**

Akizungumza na mwandishi wetu kuhusu mashindano hayo, Mbunge wa Rorya, Chege, alisema anatarajia kufanya mazungumzo na Owino ili kuona namna ya kuboresha zaidi mashindano hayo kwa kuongeza motisha.

Alisema ni jambo la heri na la kupongezwa kwa vijana wanapojitokeza kushiriki katika mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka kwa mpira wa miguu na pete wilayani humo.

"Rorya tunahimiza na kusisitiza maendeleo, na sote tunaelewa umuhimu wa vijana katika juhudi za kuleta maendeleo jimboni. Kwa sasa Peter [Owino] sio tu ni mdau wa michezo jimboni kwangu, lakini ni mdau wa maendeleo, tutaongea naye tuone namna ya kuboresha zaidi mashindano haya kwa sababu mpira sasa ni ajira kwa vijana wetu kwani kwa kutumia vipaji vyao ni nafasi nzuri," alisema mbunge huyo.

Aidha, Chege amezipongeza timu mbili za jimboni kwake Wanamaji FC ya Sota na Cofta FC ya Busurwa kwa kufanikiwa kuingia Ligi Daraja la Tatu ngazi ya Mkoa wa Mara.

Timu hizo zimepata nafasi baada ya kushinda nafasi ya kwanza na ya pili katika Ligi Daraja la Nne Wilaya ya Rorya.

Katika mchezo wa mwisho wa Ligi ya Wilaya Rorya uliochezwa katika Uwanja wa Shirati Obwere, Wanamaji FC waliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Cofta, shukrani kwa mfungaji, Riziki Abega.

Katika Ligi ya Umoja Cup 2021 inayoendelea kwenye Uwanja wa Maji Sota, ambayo msimu huu imebeba jina la mchezaji wa Wanamaji FC, Makori Odoyo (Abega wa Cameroon), aliyefariki hivi karibuni, mabingwa watetezi Kabwana FC mwishoni mwa wiki waliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Bubombi FC ya Kirongwe mpakani.

Jana ilipigwa mechi nyingine uwanjani hapo ambapo Mennonite walikuwa wenyeji wa Kabwana FC.

Katika hatua nyingine, Meneja wa Umoja Cup, Obong'o Maina, amesema mwakani wanategemea kuongeza kituo kingine kutokana na wingi wa timu na wapenzi wa soka kuongezeka kila.

"Tutakuwa na kituo Utegi, Buturi, Kowak au Kinesi ili kutoa nafasi zaidi kwa vijana wetu," alisema Obong'o.



Kikosi cha Kirengo FC, kinachoshiriki michuano ya Umoja Cup 2021. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *ATLAS yaandaa marathon kusaidia wanafunzi*

**Na Joseph Mwendapole**

SHULE za ATLAS zimeandaa mbio za nusu marathoni kwa ajili ya kusaidia wanafunzi 200 wa shule hiyo wanaosomeshwa bure kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kufiwa na wazazi, hivyo kukosa ada.

Mbio hizo zitafanyika siku ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, ambayo huadhimishwa Oktoba 14, kila mwaka, huku pia kukiwa na shughuli ya mahafali kwa wanafunzi wa shule ya awali, msingi na sekondari wapatao 750.

Ofisa Uhusiano wa shule hizo, Renalda Gilbert, alisema jana kuwa watoto hao ni wale ambao wazazi wao walifariki wakiwa wanaendelea na masomo na wazazi ambao wamepata changamoto mbalimbali kama kufukuzwa kazi au kushindwa kulipa ada kutokana na sababu mbalimbali.

Alisema mbio hizo zitakuwa za kilomita tano, 10 na 21, zitakazoanzia shuleni hapo na kuishia kwenye maeneo mbalimbali kwa kuwashirikisha wazazi, wafanyakazi na wageni watakaohudhuria siku hiyo ambayo pia itakuwa ya mahafali.

"Kuna wazazi ambao wamefariki, wengine wamepunguzwa kazi, wengine maisha yamebadilika tu wakashindwa kulipa ada, sisi ATLAS hatukuwaacha na hatutawaacha, tutaendelea nao na fedha zitakazopatikana tutawapa mahitaji muhimu ya kila siku," alisema.

Aidha, Renalda alisema wamechagua kufanya shughuli hizo siku ya kumbukumbu ya kifo cha Mwalimu Nyerere kutokana na kuamini katika falsafa yake ya uhuru na uwajibikaji kama sehemu ya kumuenzi.

Alisema Nyerere alipenda watu wawajibike kutimiza majukumu yao bila kusukumwa, hivyo ATLAS inaamini katika uwajibikaji ndiyo sababu ikaona iendelee kumuenzi kwa kufanya mahafali yake siku ambayo anakumbukwa kitaifa.

"Shule za ATLAS zimekuwa zikifanya vizuri kitaaluma katika kila matokeo ya kitaifa kuanzia shule ya msingi na sekondari, hii ni kutokana na kuamini katika falsafa ya uwajibikaji na kujituma na tunawaahidi wazazi kuwa tutaendelea kufanya vizuri watuletee watoto wao," alisema.

## Tanzanite yapania Kombe la Dunia

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kuingia hatua ya makundi katika michuano ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia mwakani nchini Costa Rica, Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Wanawake U-20 (Tanzanite), Edna Lema, amesema wapo tayari kukutana na timu yoyote katika hatua hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Edna alisema wachezaji wake walipambana katika mchezo dhidi ya Eritrea na kupata ushindi, hivyo sasa wanaenda kujipanga kwa ajili ya hatua ya makundi. Alisema bado makundi hayajapangwa na hawajui watacheza na nani, lakini kwa maandalizi watakayoendelea kuyafanya ana matarajio makubwa ya kupata matokeo mazuri.

"Sasa tunasubiri mpinzani wetu, hatujuia tunacheza na nani, kikubwa ni kuendelea kujipanga na kufanyia kazi mapungufu yetu na kuwa tayari na yoyote katika hatua inayofuata," alisema Edna Lema.

Tanzanite wamefanikiwa kuingia hatua hiyo baada ya juzi katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Eritrea hivyo kuitoka kwa jumla ya mabao 5-0 baada ya wiki iliyopita kushinda 3-0 ugenini.

## Kipa Azam ataka ushindi Pyramids

**Na Saada Akida**

KIPA wa Azam FC, Mathias Kigonya, amesema wanajiandaa vizuri na wataingia kwa tahadhari na nidhamu ya hali ya juu katika mechi dhidi ya Pyramids ya Misri ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Azam FC ambayo sasa itaikaribisha Pyramids baada ya kuitoa Horseed FC ya Somalia kwa jumla ya mabao 4-1, miamba hiyo itakutana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi wiki hii kabla ya kurudiana nchini Misri mwishoni mwa wiki ijayo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kigonya alisema ana imani mchezo huo utakuwa mgumu kwa pande zote mbili, kwa sababu wao malengo yao mwaka huu ni kuingia hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Alisema kufikia hatua hiyo lazima wapambane kutafuta matokeo mazuri katika kila mechi huku wakihitaji kutafuta ushindi mchezo huo wa nyumbani.

"Mchezo wa soka una matokeo matatu kushinda, kushindwa na kutoka sare, mwalimu ametueleza na wachezaji wote tunajua utakuwa mgumu, kwetu tunaenda kucheza na timu bora yenye wachezaji wazoefu," alisema Kigonya.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### KOULIBALY ATAKIWA

KLABU ya Newcastle United inapanga uhamisho wa mlinzi wa kati wa Napoli, Kalidou Koulibaly, 30. ***(Football Insider).***

### NESYRI KWA ARSENAL, SPURS

KLABU ya Sevilla inapima uhamisho wa mshambuliaji wa Blackburn Rovers na Chile, Ben Brereton, 22, huku Yorsef En-Nesyri, 24, akihusishwa na kuhamia Arsenal au Tottenham Hotpur. ***(Teamtalk)***

### LINGARD NAYE ATAJWA

MLINZI wa Burnley, James Tarkiwski, 28, anaweza kuwa mmoja wa wachezaji wa kwanza kusajiliwa na Newcastle, huku klabu hiyo ikiwa imemjadili mchezaji wa England, Jesse Lingard, 28, wakati mshambuliaji huyo akitarajiwa kumaliza mkataba wake na klabu ya Manchester United msimu ujao wa majira ya joto. ***(Sunday Telegraph)***

### KOCHA BRUCE KUFUKUZWA

WAMILIKI wapya wa Newcastle wanajiandaaa kumfukuza kocha, Steve Bruce wiki hii. ***(Sunday Mirror)***

### POGBA KURUDI TENA JUVE

JUVENTUS inaweza kuwa na nafasi ya kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa, Paul Pogba, ambaye mkataba wake na Manchester United uko mbioni kumalizika, ikiwa wataweza kuwauza takribani wachezaji wawili. ***(La Gazzetta dello Sport)***

### LIVERPOOL YAMTAKA DEMBELE

LIVERPOOL wanapanga kujaribu kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Ousmane Dembele kwa uhamisho huru wakati mkataba wa mchezaji huyo na Barcelona ukikaribia kuisha kipindi cha majira ya joto yajayo. ***(Teamtalk)***

### ICARDI NA NEWCASTLE

NEWCASTLE pia inavutiwa na mshambuliaji wa Paris St-Germain na raia wa Argentina, Mauri Icardi, 28, ingawa Tottenham Hotspur na Juventus pia zinamtolea macho mchezaji huyo. ***(Calciomercato, via Mail on Sunday)***

### PHILLIPS KUONGEZA MKATABA

KLABU ya Leeds United inaamini kuwa Kelvin Phillips ataongeza mkataba wake na klabu hiyo kabla ya mwishoni mwa mwaka huu, wakati mazungumzo yakiwa kwenye hatua za mwishoni. ***(Football Insider)***

### KUBORESHEWA MKATABA

MANCHESTER United inajiandaa kuanza mazungumzo na mlinzi wa kati wa England, Harry Maguire, 28, ili kuboresha masharti ya mkataba wa mchezaji huyo. ***(Sunday Mirror)***

### LACAZETTE AWANIWA INTER

INTER Milan inamfuatilia mshambuliaji wa Arsenal, Alexandre Lacazette, 30 na straika wa Real Madrid, Luka Jovic, 23. ***(La Gazzetta dello Sport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL: JORGINHO SASA ANASTAHILI BALLON D'OR

**Kwa uhakika anastahili kushinda, lakini hii ni tuzo binafsi, si kitu chenye thamani zaidi kwenye...**

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Chelsea, Thomas Tuchel, anaamini Jorginho ni mchezaji anayestahili zaidi kutwaa tuzo ya Ballon d'Or mwaka huu, lakini haamini endapo tuzo hiyo inatakiwa kuangaliwa kama muhimu sana.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, alishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na 'Blues' hao na Euro 2020 akiwa na Italia msimu uliopita na alitwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa UEFA.**

Kiungo Jorginho sasa anawania tuzo nyingine binafsi baada ya kutajwa katika orodha ya wachezaji 30 waliotangazwa kuwania tuzo ya Ballon d'Or pamoja na Lionel Messi na Robert Lewandowski.

"Kwa uhakika Jorginho anastahili kushinda Ballon d'Or," alisema Tuchel akinukuliwa na Bild.

"Hii ni tuzo binafsi, hata hivyo si kitu chenye thamani zaidi kwenye mpira wa miguu, na hatakiwi kukiwaza sana.

"Lakini ningependa mchezaji ashinde, kwa sababu inaongeza kujiamini kwa mchezaji, lakini kwa upande wangu mimi si kitu muhimu sana."

N'Golo Kante, Cesar Azpilicueta, Mason Mount na Romelu Lukaku pia wanaiwakilisha Chelsea kwenye orodha ya kuwania tuzo hiyo, na Tuchel anajisikia fahari zaidi kwa Lukaku, ambaye alirudi hapo Stamford Bridge kutoka Inter Milan Agosti, mwaka huu.

"Samahani kwa mashabiki wa Inter, lakini tulimtambua yeye kama mchezaji ambaye anaweza kutoa hamasa kubwa kwa wachezaji vijana," alisema Tuchel.

"Mara zote amesema alikuwa yupo vizuri kule Inter na (Antonio) Conte kwa sababu alifanikiwa kupata matokeo mazuri, lakini kwake yeye ilikuwa ni muhimu kurudi sehemu ambayo aliwahi kucheza wakati akiwa kijana."

Lukaku amekuwa na mwanzo mzuri hapo London, akifunga mabao manne katika mechi tisa kwenye mashindano yote msimu huu tangu alipojiunga na Chelsea.

MECHI KALI

HOME

AWAY

LIBYA

4.08 | 2.96 | 1.95

EGYPT

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money EZYPESA

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO

# TYSON FURY AMCHAPA WILDER KWA KO



**NEVADA,** Marekani

BONDIA Tyson Fury amempiga kwa mara nyingine Deontay Wilder kwa KO raundi ya 11 na kufanikiwa kutetea ubingwa wake wa mkanda wa WBC kwenye pambano lililopigwa usiku wa kuamkia jana katika Ukumbi wa T Mobile Arena, Nevada, Marekani.

Baada ya miezi 12 tangu Fury mwenye umri wa miaka 32, achukue ubingwa huo kutoka katika mikono ya Wilder, ameendeleza ubabe baada ya kumpiga katika mapambano mawili yaliyopita.

Wilder alipambana hadi raundi ya 10 akionyesha ubora wake kabla ya kudondoshwa katika raundi ya 10, na mwamuzi kusitisha pambano hilo raundi ya 11 baada ya kudondoshwa chini kwa mara nyingine.

"Nilidondoka mara kadhaa, niliumia, Wilder ni bondia mgumu," alisema Fury baada ya pambano hilo.

"Ni pambano zuri sana. Sina sababu yoyote, Wilder ni bondia bora, amenifanya nipiganie fedha zangu. Siku zote nasema mimi ni bondia bora duniani na yeye ni wa pili.



# Liverpool kumng'oa Asensio Real Madrid

**LIVERPOOL,** England

KLABU ya Liverpool imeongeza nguvu zaidi kwenye harakati za kuwania saini ya winga wa Real Madrid na Hispania, Marco Asensio mwenye umri wa miaka 25, kuelekea dirisha lijalo la majira ya baridi linalofunguliwa Januari 2022.

Asensio amekuwa akihusishwa kuondoka Real Madrid tangu dirisha lililopita kwa sababu hajisikii furaha kuendelea kusalia kwenye viunga hivyo vilivyompa jina kubwa katika soka.

Mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2023 na msimu huu amecheza mechi saba za michuano yote ambapo amefanikiwa kufunga mabao matatu.

Madrid haionekani kuwa na mpango wa kumzuia ikiwa ofa inayohitaji itawasilishwa mezani kwani Asensio mwenyewe amewaambia mabosi kwamba anahitaji changamoto mpya.

Na kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, Liverpool wanaongoza katika mbio za kuwania saini ya mchezaji huyo kwa sasa.

Ripoti hiyo imesema kwamba, Liverpool wanapanga kutoa ofa ya kumsajili mchezaji huyo wakati wa dirisha la Januari.



# Michezo

Jumatatu Oktoba 11, 2021
Nipashe



## Tuchel: Jorginho anastahili Ballon d'Or

UKURASA 21



Winga wa Taifa Stars, Simon Msuva, akiwatoka mabeki wa Benin kabla ya kuachia shuti kali lililojaa moja kwa moja wavuni na kuifanya Tanzania kuibuka na ushindi wa bao 1-0 kwenye mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar iliyopigwa Uwanja wa L'Amitie, Cotonou, Benin jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

### Makocha wa4 Ulaya waliokalia kuti kavu

**LONDON,** Uingereza

MAKOCHA wanakuwa wa kwanza kukosolewa pale timu inapokuwa na matokeo mabaya...



HABARI UK. 11

### Xavi: Nipo tayari kurudi Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

XAVI amesema amefungua mlango kuhusu uvumi unaomhusisha yeye kuchukua nafasi ya...



HABARI UK. 23

# Stars yatoa shoo ya kibabe Benin

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Manula shujaa wa mchezo, Msuva awalaza Wabenin mapema tu, Tanzania yakaa kileleni huku...

USHUJAA ulioonyeshwa na mlinda mlango wa timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Aishi Manula, huku winga Simon Msuva akitekeleza majukumu yake vema ya kuliona lango la Benin kwenye mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia Qatar 2022, liliifanya Stars kuibuka na ushindi wa bao 1-0 jana.

**Bao la dakika ya sita lililofungwa na winga wa kimataifa wa Tanzania anayeichezea Klabu ya Wydad Casablanca ya Morocco, Msuva, ndilo lililowafanya Wabenin hao jana kulazimika kulala mapema tu baada ya mchezo huo uliopigwa Uwanja wa L'Amitie, Cotonou nchini Benin.**

Stars imelipiza kisasi cha kufungwa bao 1-0 nyumbani, Alhamisi iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, hivyo kupindua meza ugenini kibabe.

Katika mchezo huo Stars ilikuwa nyuma ya mpira kwa muda mrefu, huku kipa Manula akiibuka shujaa kwa kuokoa michomo na hatari nyingi kutoka kwa wachezaji wa Benin.

Ulikuwa ni mpira wa kurushwa na Israel Mwenda pembeni mwa uwanja alimrushia Msuva, ambaye aligeuka na kuanza kuwalamba chenga mabeki wawili wa Benin, kabla ya kuachia shuti kali lililokwenda moja kwa moja hadi wavuni, lilimwacha kipa Saturnin Aliagbe akiwa hana la kufanya.

Baada ya bao hilo la mapema, Stars ilionekana kurudi nyuma na kuanza kujilinda, mbele ikimwacha Kibu Denis na wakati mwingine akisaidiana na nahodha Mbwana Samatta.

Manula aliiweka salama Stars dakika mbili kabla ya mapumziko, baada ya Djallilou Ouorou kupenyezewa pasi safi ndani ya eneo la hatari, na kupiga shuti kali ambalo aliliokoa kwa mguu wa kushoto, kabla ya mpira huo kufagiliwa mbali na Bakari Mwamnyeto.

Kipindi cha pili, Kocha Mkuu wa Stars, Kim Poulsen alifanya mabadiliko, akiwatoa Kibu, Feisal Salum, Msuva na kuwaingiza, Ralients Lusajo, Zawadi Mauya, na Abdul Selemani, ambaye naye baadaye alitolewa na nafasi yake kuchukuliwa na Edward Manyama.

Chabel Gomes, nusura aisawazishie Benin bao dakika ya 53, alipiga kichwa mpira wa krosi, lakini Manula alichupa na kuudaka kwa ustadi wa hali ya juu.

Mchezaji hatari aliyeisumbua ngome ya Stars kwenye mechi ya kwanza Dar es Salaam, Michael Pote, ambaye hata kwenye mchezo wa jana alionekana kufurukuta, aliingia ndani ya eneo la hatari na kuachia shuti kali, lililookolewa na Manula dakika ya 59.

Dakika nne baadaye krosi ya Steve Mounie aliyefunga bao pekee nchini, ilikuwa ikisubiriwa na wachezaji wawili wa Benin, David Kiki na Mateo Ahlinvi waliielekeza wavuni, lakini kipa huyo aliruka na kudaka kwenye miguu ya wachezaji hao ambao, wakiishia kuingia nyavuni, mpira ukibaki salama mikononi mwa Manula.

Kwa matokeo hayo ya jana, Stars ilirudi kileleni kwa muda, ikiwa imefikisha pointi saba kama Benin, lakini ikiwa na mabao mengi ya kufunga, ikisubiri mechi iliyotarajiwa kuchezwa jana usiku kati ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ambayo ilikuwa ugenini dhidi ya Madagascar.

Sare yoyote au kipigo kwa DR Congo, kutaifanya Stars kuendelea kutanua juu, lakini ushindi kwa Wakongomani hao wenye pointi tano utawafanya kwenda kileleni kwa kufikisha pointi nane.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >